**Serikali** sasa kuajiri wataalamu 800 wa kuisaidia TAKUKURU

UKURASA 5

**Kiama** chaja kwa waajiri wasiopeleka michango mifuko hifadhi ya jamii

UKURASA 2




UKURASA 9


# Nipashe

Jumapili Julai 9, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

JUMAPILI

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0581366

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# Balozi Karume ataja kinachofuata baada ya kufukuzwa CCM

• **Ateta** na Nipashe Jumapili, adai anatilia shaka kikao kilichoitishwa usiku wa manane... *Endelea Ukurasa. 3*

## YALIYOMO


UKURASA WA 7

### TUNYOE NYWELE, TUFUE NGUO KUEPUKA 'CHAWA' WA WATU

UKIAMKA asubuhi ukakutana na mtu akusalimu 'we mbwa hujambo?' Utamjibu au utakaa kimya huku ukiugulia hasira?...

UKURASA WA 11

### UFANYE NINI UNAPOISHI NA MKWE MUDA MREFU?



KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada yetu ya mama mkwe. Makala tatu hivi mfululizo zilipata wachangiaji...


## Waziri awaagiza polisi kukamata wanaotoa kauli hatari kiusalama

UKURASA 3




## Majaliwa: Hatutomwacha DP World aende zake

UKURASA 2


MICHEZO NI VITA NGAO YA JAMII UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (wa pili kushoto), Mbunge wa Ilala Mussa Zungu (wa pili kulia), Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kudilamoto (kushoto), wakiwa katika ziara ya kutatua changamoto ya malipo kwa wananchi wanaotakiwa kufidiwa eneo baada ya kupisha utanuzi wa uwanja wa ndege, Kata ya Kipawa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaliwa ataja msimamo wa serikali uendelezaji Bandari

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inaendelea na mpango wa kuikabidhi Bandari ya Dar es Salaam kwa mwekezaji ambaye ni kampuni ya DP World ya Dubai na kusisitiza kuwa maoni ya watanzania yatazingatiwa.

Katika mkutano na wananchi wa mjini Mtwara juzi, Majaliwa alisisitiza kuwa hadi sasa kilichotiwa saini ni makubaliano ya awali na muda ukifika maoni ya wananchi yatazingatiwa.

"Hatuwezi kumwacha huyu (DP World) aende zake. Kilichopitishwa na Bunge si mkataba wa miradi ni makubaliano ya awali baina ya nchi ili kuruhusu uwapo wa mikataba ya miradi husika, hivyo katika mikataba hiyo maoni yenu yatazingatiwa," alisisitiza.

Akifafanua baadhi ya hoja zinazotolewa na wanaopinga makubaliano hayo, Majaliwa alisema "maeneo ambayo mna shaka nayo, mnasema mkataba huu ni wa kudumu, sisi tunasema bado. Kwenye mkataba huo tutaweka muda wa kumfanyia tathmini (mwekezaji) aendelee au la, kwa sababu hata huyo aliyeondoka mwaka jana naye tulimpa muda wa vipindi mpaka akafikia miaka 22.

"Uwekezaji pale (bandarini) siyo suala geni, siyo kitu kipya. Mmesema tuzingatie maslahi ya Taifa, ninataka niwahakikishie kwamba mkataba utazingatia maslahi ya taifa hili. Serikali yenu ni sikivu," alisema.

Akijibu hoja ya ardhi kwamba mwekezaji huyo ameichukua, kiongozi huyo alisema "mmesema ardhi ameichukua, itakuwa ya kwake... hapana! Hakuna mwekezaji aliyepewa ardhi, hata sheria za uwekezaji, mwekezaji hapewi ardhi, bali anapata kibali cha kukaa juu ya ardhi na akikaa hapo atalipa kodi," alifafanua.

Kuhusu muda wa mkataba ambao baadhi ya wadau walisema mwekezaji huyo amepewa kwa miaka 100 na wengine miaka yote, Majaliwa alikanusha na kusema halijatamkwa kokote.

Alisisitiza mwekezaji huyo atakapokuja watakubaliana miaka ya kukaa na kufanya tathimini kama ni miaka mitano kisha mitano tumwangalie au kama ni miaka 10.

Akifafanua hoja ya watu kupoteza ajira, Majaliwa alisema hakuna mtumishi wa bandari ambaye atapoteza ajira yake.

"Hofu nyingine wamesema serikali haitapata hata senti tano kwa hiyo huyo anakuja kukaa hapa anaondoka hatupati hata senti tano. Kwani sisi hatuwezi kusimamia maslahi ya watanzania kweli? Huyu tumlete hapa asilipe hata senti tano kweli? Haiwezekani lazima alipe kodi.

"Watanzania wenzangu tuamini jambo hili linakokwenda litaleta maslahi kwa taifa na serikali itazingatia maslahi ya watanzania. Tatizo ni kwamba watu wanasema bandari yote, siyo kweli.

"Sisi tunalenga sehemu ya kupakia na kushushia. Meli nyingi zinashindwa kuingia pale kwa sababu mitambo tuliyonayo ni midogo midogo ya kushusha na kupakia, haishushi kwa haraka," alifafanua.

Majaliwa alisisitiza kuwa hakuna mahala wanataka kudhuru watanzania na kuomba waiamini serikali kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ana nia njema ya kufungua milango kiuchumi.

"Maeneo haya matano yenye wasiwasi tunayafanyia kazi kwa hiyo kilichopitishwa na wabunge si mkataba na DP World, bali makubaliano ya nchi na nchi ili kuruhusu kuzungumza," alifafanua.

Alisema serikali inatarajia kujenga reli ya kisasa (SGR) ambayo itaunganisha Bandari ya Mtwara na mikoa mingine ili kuufungua ushoroba wa mkoa huo.

"Tutajenga reli ili kuiunganisha bandari yetu na migodi ya makaa ya mawe kule Liganga, Nchuchuma na nyingine itakwenda Iringa ili kuifungua Mtwara," alisema.

Mbunge wa Mtwara Mjini, Hassan Mtenga, aliiomba serikali kuhakikisha korosho zinasafirishwa kupitia Bandari ya Mtwara ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

"Kuna vijana tangu saa 12 asubuhi hadi saa sita usiku wako kwenye makundi ya mtandaoni (WhatsApp) kutukana viongozi, hili ni kwa sababu hawana kazi ya kufanya.

"Iwapo korosho zetu zitasafirishwa kupitia bandari yetu, vijana hawa watapata ajira na kuacha kutukana viongozi," alisema.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 157 kutekeleza mradi ujenzi wa gati jipya la Bandari ya Mtwara.

"Uwekezaji huu umelenga kuifanya Bandari ya Mtwara kuwa ya kimkakati na sasa inaweza kufunga meli zaidi ya nne kwa wakati mmoja.

Haya ni maendeleo makubwa," alisema.

Waziri wa Ofisi ya Rais - Kazi Maalum, Kapteni mstaafu George Mkuchika, aliwataka wananchi wa Mtwara kutoyaogopa mabadiliko ya uendeshaji wa bandari na badala yake waiunge mkono serikali.

"Msiogope na wala msiwe na wasiwasi, ni tabia ya mwanadamu kuogopa mambo mapya, suala la uwekezaji katika bandari siyo geni," alisema Mkuchika.

Majaliwa yupo mkoani Mtwara kwa ziara ya kikazi na jana alitembelea Halmashauri ya Mtwara na Mji wa Nanyamba.

## Kiama chaja waajiri wasiopeleka michango mifuko hifadhi ya jamii

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imetangaza kuchukua hatua za kisheria dhidi ya waajiri wote wa sekta binafsi na wa mamlaka za serikali wenye madeni na wanaochelewesha kuwasilisha michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alitangaza mpango huo juzi baada ya kutembelea mabanda ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF, PSSSF na WCF katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara, maarufu Sabasaba, yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere mkoani Dar es Salaam. Katambi aliwaagiza waajiri wote nchini, wakiwamo wa mamlaka za serikali na sekta binafsi kuhakikisha wanawasilisha kwa wakati michango ya wanachama katika mifuko ya NSSF, PSSSF na WCF sambamba na kulipa madeni yao.

"Ninawaagiza waajiri wote nchini kuwasilisha michango ya wanachama wao kwa wakati ili wastaafu ambao wamelitumikia Taifa hili kwa utumishi uliotukuka na kwa heshima kubwa, katika uzee wao wasianze kunyanyaswa.

"Hatutakubali wazee wetu waanze kuhangaika kisa mwajiri wake hajawasilisha michango. Tutachukua hatua za kisheria kwa waajiri wa sekta binafsi na waajiri wa mamlaka za serikali tunakwenda kuwashtaki kwa Mheshimiwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan," alisema Katambi. Naibu Waziri huyo aliomba kupatiwa orodha ya waajiri wote ambao wanadaiwa malimbikizo ya michango sambamba na wasiowasilisha michango ya wanachama wao ili wachukuliwe hatua mara moja na ikibidi watawatangaza hadharani.

Pia, aliwaagiza waajiri kulipa mishahara ya wafanyakazi wao kwa kuwa ni matakwa ya kisheria. Alisema baadhi ya kampuni hazilipi mishahara kwa wakati, jambo ambalo ni kinyume cha sheria za nchi, hivyo akawataka kuacha tabia hiyo mara moja.

Katambi pia aliiagiza mifuko ya hifadhi ya jamii kuendelea kuandikisha wanachama wengi zaidi ili mifuko iendelee kuwa na manufaa makubwa huku akiitaka kuangalia kwa umakini ushauri unaotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) wa kufanya utafiti mkubwa kuangalia miradi na uwekezaji wenye tija ili kulinda thamani ya fedha za mifuko.

Alisema miongoni mwa mikakati ambayo inafanyika serikalini ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na mazingira mazuri na stahiki katika masuala ya kiuchumi na kulinda afya zao.

Katambi alisema NSSF ni mfuko pekee unaotoa huduma kwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na kwamba hivi sasa umetengeneza skimu mbalimbali ambazo zitawagusa Watanzania wote wakiwamo mama lishe, bodaboda, wakulima, wavuvi, wafugaji, wachimbaji wadogo wa madini na wajasiriamali wengine wote.

Alisema mfuko umewekeza katika maeneo mbalimbali na uwekezaji huo umechangia ukwasi na kufikia Sh. trilioni 7.1. Akatumia fursa hiyo kuwahamasisha NSSF kuzidi kuwekeza katika maeneo salama na yenye faida.

"Ninatambua NSSF mnawekeza vizuri, mmewekeza kwenye Daraja la Nyerere, Kigamboni ambalo hivi sasa wananchi wanapita kwa bei nafuu sana baada ya agizo la Mheshimiwa Rais Samia la kuwaondoshea kero wananchi," alisema.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alisema mfuko unaendelea kuwakaribisha wanachama na wadau kutembelea banda namba 13 ili wapate elimu ya hifadhi ya jamii, taarifa za michango, taarifa kuhusu uwekezaji na taarifa kuhusu mafao.

Lulu alisema wananchi wote ambao watatembelea banda hilo pia wataweza kupata fursa mbalimbali za NSSF zikiwamo za nyumba na viwanja ambavyo vinauzwa katika maeneo mbalimbali. Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma, alisema mifuko yote iko vizuri na itaendelea kutoa huduma kwa weledi katika kukusanya michango na kutoa mafao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Zanzibar (ZEA), Juma Buruhani Mohammed, alisema amefarijika kupata fursa ya kujionea shughuli za mifuko hiyo.

Mmoja wa waajiri, Isani Longo, kutoka kampuni ya Elfatel Enterprises Company Limited iliyoko Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, alisema ni mmoja wa waajiri ambao mfanyakazi wake aliumia akiwa kazini na amepata huduma za utengamao kutoka WCF na amelipwa fidia.

## HABARI KITAIFA



Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Godius Kihyarara, akipata maelezo kutoka kwa Mhadhiri wa Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Crezencia Massawe kuhusu Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya na Bodi za Afya za Halmashauri zinazosimamia utoaji wa huduma za afya katika vituo vya afya na hospitali za wilaya nchini, kwenye Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, maarufu Sabasaba. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Balozi Karume ataja kinachofuata baada ya kufukuzwa CCM

**Na Waandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MUDA mfupi baada ya uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutangaza kumfuta uanachama mtoto wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Balozi mstaafu Ali Abeid Karume, kupitia kikao cha usiku wa manane, mwenyewe aibuka na kusema atakata rufani kupinga uamuzi huo.

Akitangaza uamuzi huo uliotokana na maazimio ya kikao cha Halmaushauri Kuu ya CCM Mkoa wa Kusini Unguja kilichofanyika saa saba usiku wa kuamkia jana, Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM mkoa huo, Ali Timamu Haji, alisema kuwa mbali na uamuzi huo, pia wanamtaka Balozi Ali arejeshe kadi waliyompatia.

Ni uamuzi uliofanyika muda mfupi baada ya kada huyo kuzungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake na kukishutumu chama chake kuwa na utaratibu anaopingana nao - watu wasio na uzoefu kupewa nafasi za uongozi serikalini.

Haji alisema uamuzi huo umetokana na mwenendo wa kada wao huyo kukiuka maelekezo ya maadili, miongozo na nidhamu.

Juzi, kada huyo, mbele ya waandishi wa habari, alikishauri chama hicho kuepuka kufanya alichokiita makosa ya uteuzi kwa wanachama wake ambao hawajawahi kushika nafasi za chini za kisiasa na kiserikali kupewa nyadhifa za juu.

Alionya kwamba uteuzi wa aina hiyo unasababisha chama hicho kupata viongozi aliowaita dhaifu, wasiojua maana ya siasa, uongozi na utawala.

Mwandishi alipomtafuta Balozi Ali jana kuzungumzia uamuzi wa kufukuzwa CCM, alisema ameona taarifa hiyo katika mitandao ya kijamii, kwamba CCM Mkoa wa Kusini Unguja kupitia Kamati ya Halmashauri Kuu ya CCM, imemfukuza uanachama. Hajapokea barua yoyote.

Balozi Ali alisema hana mpango wa kurejesha kadi ya CCM wala kwenda chama kingine cha siasa.

Alisema kwa sasa anasubiri barua hiyo na atakapoipata, atakata rufani ya kupinga uamuzi katika Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu Taifa ya CCM kwa sababu ni haki yake ya kikatiba.

"Nimesikia kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii uamuzi uliochukuliwa, sijaitwa, wala kupewa nafasi ya kujieleza. Lakini kama uamuzi umeshapita, ninasubiri barua rasmi ili nikate rufani kwa sababu nina haki yangu," alisema.

Balozi Ali alisema ana wasiwasi juu ya uhalali wa kikao cha Halmashauri Kuu ya Mkoa kilichotoa uamuzi wa kumfukuza uanachama wake.

**UAMUZI WA CHAMA**

Akitangaza uamuzi huo, Haji alisema umefikiwa kwa mujibu wa Katiba ya CCM ya mwaka 1977 toleo la mwaka 2022.

Alisema uamuzi huo ni kwa mujibu wa Ibara ya 89 inayoeleza kazi za Halmashauri Kuu ya Mkoa inayoelekeza kuangalia mienendo ya wanachama na viongozi wa CCM wa ngazi ya mkoa kichama na kulazimika kutoa taarifa kwa vikao vinavyohusika ngazi za juu.

Pia, alinukuu Ibara ndogo ya 14 kifungu kidogo cha 14, ambacho kinaelekeza kumwachisha au kumfukuza uanachama mwanachama yeyote endapo itadhihirika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za uanachama wake.

Kadhalika, alisema kifungu hicho kinasema mwanachama anayeachishwa au kufukuzwa uanachama anaweza kukata rufani kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa.

Timamu alisema kutokana na kupewa nguvu na Katiba ya CCM, waliotoa uamuzi walijiridhisha kwa kina kuhusu madai ya kukiuka maelekezo ya kikatiba na kupitia mapendekezo yote yaliyopokewa kutoka ngazi za tawi, wadi, jimbo na wilaya ambazo ni ngazi za chini za mkoa huo.

Alisema Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa huo imeridhia na kuridhika kwamba kutokana na kauli na vitendo vya mwanachama huyo, wamekubaliana kumwachisha uanachama wa CCM na kumtaka arudishe kadi ya uanachama ya kielektroniki namba C000/2809/993/1 ya Machi 17 mwaka 2022.

"Mwanachama huyu ameitwa na kuonywa kwa maandishi na vikao mbalimbali vya CCM, lakini hakutii wala kubadilisha tabia na vitendo vyake na kuendelea kukiuka kwa makusudi maadili na miongozo ya CCM.

"Hivyo, kwa mamlaka tuliyopewa na Katiba yetu ngazi ya Mkoa ya CCM Kusini Unguja, kwa kauli moja tumefikia uamuzi na makubaliano ya kumwachisha na kumfukuza uanachama mwanachama huyu," alisema.

**WASIFU WAKE**

Balozi Ali amewahi kushika nafasi mbalimbali za chama na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwamo kuwa Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya, Mkoa, Mwakilishi wa kuteuliwa, Waziri wa Mawasiliano, Ujenzi na Uchukuzi Zanzibar, Waziri wa Vijana na Michezo Zanzibar na Balozi wa Tanzania katika nchi mbalimbali.

Balozi Ali alizaliwa Mei 24, 1950. Ni mtoto wa kwanza wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Mzee Abeid Amani Karume, pia ni ndugu wa Rais mstaafu wa Awamu ya Sita Zanzibar, Amani Abeid Karume.

Mwaka 2005 na 2010 alijitosa kugombea uteuzi wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kupeperusha bendera ya CCM, lakini hakuteuliwa.

Akiwa na miaka 28, aliteuliwa kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Biashara na Viwanda katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kazi aliyoishikilia kwa miaka sita (1972 - 1978) alipoomba likizo na kwenda kujiendeleza zaidi kimasomo Marekani.

Balozi Ali alianza kufanya kazi za kibalozi mwaka 1989 alipokuwa Balozi wa Tanzania na Marekani.

Mwaka 1993 alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Masuala ya Ulaya na Marekani katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya Tanzania hadi mwaka 1996 alipopelekwa Ubelgiji kuwa Balozi wa Tanzania kwa nchi za Ubelgiji, Uholanzi, Luxembourg na Umoja wa Ulaya.

Mwaka 2002 alikuwa Balozi wa Tanzania katika nchi za Ujerumani, Uswizi na Poland sambamba na kuangalia uhusiano na nchi za Australia, Jamhuri ya Czech, Slovakia, Hungary, Romania na Bulgaria.

Kuanzia mwaka 2006, aliteuliwa na Rais Jakaya Kikwete kuwa Balozi wa Tanzania katika nchi za Italia, Ugiriki, Uturuki na Malta. Pia amekuwa Balozi wa Tanzania Cyprus na Mkuu wa Mabalozi wa Tanzania.

***Imeandaliwa na Rahma Suleiman na Is-Haka Omar**

## Waziri aagiza polisi kukamata wanaotoa kauli hatari kiusalama

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amelitaka Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua wale wote wanatoa kauli za kuhatarisha usalama wa nchi.

Masauni alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari na kusema kuwa kuna baadhi ya watu wanatoa kauli za kuhatarisha usalama wa nchi kutokana na uhuru waliopewa.

Alisema kutokana na uhuru waliopewa, wananchi wanatakiwa kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa sheria za nchi kwa kuwa viongozi hawatovumilia vitendo hivyo.

"Ninalielekeze Jeshi la Polisi kuhakikisha hawafumbii macho mtu yeyote au kikundi chochote kitakachosababisha au kwa vitendo au kauli katika kuvunja sheria za nchi yetu na kuhatarisha usalama, wachukuliwe hatua," aliagiza Masauni. Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anaendelea kufanya kazi nzuri kuimarisha demokrasia na uhuru, hivyo wananchi wasiutumie uhuru huo vibaya.

"Tutaendelea kupokea ushauri na mawazo yatakayotolewa lakini kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya Watanzania wenzetu wameanza kutumia uhuru huo vibaya na kutoa kauli ambazo zinalenga kuhatarisha usalama wa nchi, kuvunja sheria za nchi na kulipasua taifa, kauli hizo haziwezi kukubalika," alisisitiza.

Masauni alisema haiwezekani mtu kutumia kisingizio cha uhuru kutoa maoni yanayolenga kuvunja sheria za nchi, kwa kuwa wana wajibu wa kuhakikisha sheria zinalindwa kwa maslahi ya nchi.

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**WU ZHOU INVESTEMENT COMPANY LIMITED** inatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yeye usajili namba **T988 CYA,** Chassis No. **LBRSPJB54E9010080** na Engine No. **14918808.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**SIM/MAS/RB/229535/2023**

217488702

# SABASABA KATIKA PICHA



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi (wa kwanza kushoto), akishuhudia mwanachama wa NSSF anavyopata huduma katika banda la mashirikiano kati ya NSSF na PSSSF wakati alipotembelea maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa 'Sabasaba' yanayoendelea jijini Dar es Salaam. Katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, na Kulia ni Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Mwenyekiti wa Kampuni ya Daftari la Mama, Steven Mongere (kulia), Mhamasishaji wa Daftari hilo, Masha Ngumbi (Katikati) na Mwenyekiti Msaidizi wa Kampeni ya Daftari la Mama, Philomena Mwalongo (Kushoto) wakizindua Daftari Maalum la Mama litakalogawiwa bure mashuleni Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: IMANI NATHANIEL**




Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Haba (kushoto), akizungumza na watumishi wa Hifadhi ya Ngorongoro wakati alipotembelea banda la wizara hiyo katika maonesho ya 47 ya biashara sabasaba jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wananchi wakiangalia Kobe katika mabanda ya Wizara ya Maliasili na Utalii katika maonesho ya 47 ya biashara sabasaba jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Meneja Uzalishaji wa Umoja wa wauza Asali nje ya nchi, Kaziregе Camara (kulia), akimueleza jambo, Meneja mipango wa Ulaya EU Dk. Mathew Mapunda, wakati alipotembelea banda la Asali Asili katika maonesho ya Kimataifa ya 47 Biashara ya Sabasaba kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Kariakoo, Martine Mbwana (kulia), akipata Maelezo kutoka kwa Ofisa Foroza Mwandamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Chagula Gervas, masuala mbalimbali ya kodi alipotembelea Banda lao katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara viwanja vya Sabasaba barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## HABARI KITAIFA




Wafanyabiashara wa Mafuta ya kunukia Pafyum wa Kampuni ya Mwamwamwamwa kutoka Zanzibar kulia wakiwapa maelezo wateja waliotembelea banda la Zanzibar katika Maonesho ya 47 ya Biashara Sabasaba Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali kuajiri wataalamu 800 kuisaidia TAKUKURU

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imesema kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), itaajiri maofisa 800 wenye taaluma mbalimbali kwa lengo la kwenda kudhibiti upotevu wa fedha za umma hasa miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema maofisa hao watasambazwa maeneo mbalimbali nchini ili kukabiliana na vitendo vya rushwa katika miradi ya serikali inayotekeleza.

"Ninakiri kuwa kuna upungufu na ubadhirifu katika miradi mingi inayotekelezwa ikiwamo ile ya kimkakati, hivyo serikali imeamua kuongeza nguvu ili kudhibiti ubadhirifu huo kwa kuongeza maofisa hawa watakaotawanywa wilaya zote,"alisema.

**NDEGE YAACHIWA**

Kuhusu ndege ya Kampuni ya ndege Tanzania (ATCL) aina ya Airbus 202 iliyokuwa inashikiliwa Uholanzi, Msigwa alisema tayari imeshaachiwa na iliwasili juzi na kufanya idadi ya ndege za shirika kufikia 15.

Alisema, ndege hiyo imeachiwa baada ya jitihada mbalimbali za serikali kufanyika huko.

"Chuma kimetua Tanzania. Kutokana na ujio wa ndege hii, kumeongeza idadi ya ndege zetu zinazomilikiwa na Shirika la ATCL. Mkakati wa serikali ni kuhakikisha inatoa huduma bora za usafiri wa anga ikiwamo usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi," alisema.

Ukirejewa mgogoro uliosababisha kushikiliwa kwa ndege hiyo, mnamo Desemba 2022, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, alikiri kampuni ya Eco Development Group ya Sweden kushinda tuzo ya dola za Marekani milioni 165 (Sh. bilioni 398) dhidi ya Tanzania na hivyo kushikilia ndege hiyo.

Dk. Feleshi alisema ndege hiyo haiwezi kupigwa mnada kutokana na rufani ya kesi iliyokuwa inaendelea katika Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID).

Kituo hicho chini ya majaji watatu; Sir Christopher Greenwood, Stanimir Alexandrov na Funke Adekoya, kilitoa tuzo kwa Eco Development na kuamuru Tanzania kulipa kiasi hicho cha fedha, Aprili mwaka jana.

Mnamo mwaka 2017, Eco Development Group, inayomilikiwa na raia 18 wa Sweden, iliwasilisha madai ya usuluhishi ya dola milioni 500, ikilalamikia uamuzi wa Serikali ya Tanzania kufuta umiliki wa ardhi ya mradi wake wa sukari wa Bagamoyo. ICSID ilibariki tozo ya dola milioni 165 badala ya dola milioni 500.

Wizara ya Ardhi kupitia Kamishna wa Ardhi iliieleza kampuni hiyo Novemba 2017 kuwa serikali iliazimia kufuta hati miliki ya hekta 20,400 kwa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Msigwa pia alisema ndege za kimataifa zaidi ya 10 zinatua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) ikiwa ni sawa na asilimia 60 ya watalii wanaoshushwa kuja kuona vivutio mbalimbali nchini.

"Serikali imefanya jitihada kubwa kwenye kuliongezea uwezo shirika ili litoe huduma bora, japo bado halijaanza kutoa faida lakini huduma zinazotolewa ni bora," alisema.

Msigwa alitaja mkakati mwingine wa serikali wa ujenzi wa ukumbi wa kisasa wa mikutano utakaoitwa, 'Mount Kilimanjaro Conference Center' unaotarajia kujengwa eneo la Kijenge jijini Arusha kupitia Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC).

Alisema ukumbi huo ambao unatarajia kujengwa wakati wowote kuanzia sasa, utakuwa na uwezo wa kubeba watu 3,000 na ndani yake kutakuwa na hoteli yenye hadhi ya nyota tano na maduka makubwa.

Alisema utakapokamilika utakuwa ni moja ya kichocheo cha utalii wa mikutano kwa kuwa jiji hilo ni kitovu cha utalii nchini.

"Tunataka kuitendea haki Tanzania kwa kuongeza kumbi za mikutano na tuwe bora Afrika kwenye eneo hili, ndiyo maana serikali tunawekeza zaidi katika eneo hilo.

"Faida kubwa ukiitaka katika masuala ya utalii ni lazima kuwa na ndege zenye uhakika na ndiyo sababu hapa tunaongeza idadi ya ndege na tayari ya mizigo tunayo," alisema.

Msigwa ameyasema hayo wakati Tanzania ikiwa mwenyeji wa maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Rushwa katika Bara la Afrika katika ukumbi wa mikutano AICC.

## 'JKT inatekeleza maagizo ya Rais'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kesho, amesema JKT itaendelea kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuibua na kutambua vipaji vya vijana na kuviendeleza.

Bashungwa aliyasema hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho hayo yanayotarajiwa kufanyika kesho, mgeni rasmi akitarajiwa kuwa ni Rais Samia.

Alisema katika maadhimisho hayo, Israel imealikwa kushiriki kutokana na historia ya ushirikiano ulioanza enzi za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alipokuwa anakwenda Ghana kwa shughuli za kiserikali, aliongozana na baadhi ya marafiki, viongozi wa nchi hiyo na aliporejea ndipo JKT ilianzishwa.

Pia alisema, viongozi mbalimbali wamealikwa kuhudhuria maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo tangu lianzishwe Julai 10, 1963 na kuomba watanzania wajitokeze kwa wingi kujionea gwaride litakalofanywa na vijana wa JKT pamoja na shughuli mbalimbali za kijamii.

"JKT itaendelea kutekeleza agizo la Rais Samia la kuibua na kutambua vipaji vya vijana ikiwamo kuviendeleza ili kuwajengea uwezo katika fani mbalimbali," alisema.

Waziri Bashungwa alisema pamoja ulinzi wa taifa, jeshi hilo lina jukumu la kulea vijana katika maadili na uzalishaji mali kupitia Shirika la Uzalishaji Mali ( Suma JKT) linalowaandaa kuwa bora.

Alisema moja kati ya maagizo ya Rais Samia kwa JKT ni kuibua, kulea na kukuza vipaji vya vijana hususani wanaolelewa ndani ya jeshi hilo ili wajitambue na kuwa imara.

Alisema maadhimisho hayo yalitanguliwa na shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo uzinduzi wa mnara wa kumbukumbu ya miaka 60, uchangiaji wa damu, kutembelea vituo vya kulea watoto na kutoa zawadi mbalimbali vikiwamo vyakula na kufanya usafi katika Hospitali ya Chamwino na kutoa msaada kwa wagonjwa.

# TCRS yagawa majiko banifu kukabili uharibifu mazingira

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SHIRIKA la Kikristo la Kuhudumia Wakimbizi la Tanganyika (TCRS) limegawa majiko banifu 7,200 kwa wakazi wa kata nne zilizopo wilaya ya Morogoro ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

Ofisa Mwezeshaji wa TCRS, Gasper Werema, alisema kuwa majiko hayo yamekuwa msaada katika kuleta uhifadhi na kupunguza uharibifu wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema, jana mjini hapa kuwa majiko hayo yanatumia kuni chache tofauti na mengine ambayo hutumia mkaa na kuleta uharibifu mkubwa wa misitu.

Alisema TCRS imekuwa ikitoa elimu kupitia wawezeshaji wao waliopo katika vijiji 15 vya kata nne wilayani hapa na mpaka sasa wana waraghibishi sita waliowezesha kupatikana wengine wanne kila kijiji ambao hutoa mafunzo kwa wanakijiji, namna ya kuyajenga majiko ili kupunguza ukataji hovyo wa miti.

Balozi wa Mazingira Ofisi ya Makamu Rais, Muungano na Mazingira, Chage Alex, alisema ni vyema suala la uhifadhi wa mazingira likapewa nafasi kubwa katika jamii kwa sababu kupitia mawaziri wa kisekta ikiwamo mazingira na nishati wameweka maazimio ya kufanya nchi kuondoka kwenye matumizi ya kuni na mkaa na kuingia kwenye nishati safi ya kupikia.

Alisema takwimu zinaonesha watu wengi wanapata maafa kila mwaka kutokana na athari za moshi wanaovuta ikiwamo kupata magonjwa kama saratani na Kifua Kikuu (TB).

Alisema jamii inapaswa kuzingatia ajenda muhimu ya mazingira ya utunzaji vyanzo vya maji, udhibiti wa taka ngumu, nishati safi ya kupikia, kuondoka kwenye matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema ifikapo mwaka 2024, serikali imeazimia shule zote na taasisi za umma zinazohudumia kuanzia watu 100 hadi 300 kupigwa marufuku kutumia kuni na mkaa sababu zinachangia upotevu wa tani hekta 469,000 za misitu kwa mwaka wakati zilizopo ni hekta milioni 148.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waajiri wasiopeleka michango mifuko ya hifadhi ya jamii wachukuliwe hatua

**WASTAAFU** kutolipwa mafao yao kwa wakati kimekuwa kero ya muda mrefu. Kiini cha tatizo ni waajiri kutowasilisha michango kwa wakati katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Kumekuwa na karipio toka kwa viongozi waandamizi serikali dhidi ya waajiri, wakionywa kutochelewa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao katika mifuko husika.

Juma hili serikali kupitia Ofisi ya Waziri inayosimamia mifuko hiyo, imetangaza kuchukua hatua za kisheria dhidi ya waajiri wote wa sekta binafsi na wa mamlaka za serikali wenye madeni na wanaochelewesha kuwasilisha michango ya wafanyakazi katika mifuko hiyo.

Ni hatua iliyotangazwa juzi na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alipotembelea mabanda ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF, PSSSF na WCF katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara, maarufu Sabasaba, yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere mkoani Dar es Salaam.

Kiongozi huyo aliagiza waajiri wote nchini kuwasilisha michango ya wanachama wao kwa wakati ili wastaafu ambao wamelitumikia Taifa kwa heshima, katika uzee wao wasianze kunyanyaswa.

Aliomba kupatiwa orodha ya waajiri wote ambao wanadaiwa malimbikizo ya michango sambamba na wasiowasilisha michango ya wanachama wao ili wachukuliwe hatua mara moja na ikibidi watawatangaza hadharani.

Nipashe Jumapili, tukiwa wadau wa kuhamasisha uwajibikaji serikalini na sekta binafsi, tunaunga mkono hatua hiyo ya serikali kwa kuzingatia kilio cha muda mrefu cha wastaafu kutopata mafao yao kwa wakati.

Tunafahamu kwamba ripoti ya 2020/21 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), mbali na mambo mambo mengine, ilikuwa na taarifa za kina kuhusu kadhia hii.

CAG katika ripoti yake hiyo, ana orodha ya halmashauri na taasisi za serikali zisizowasilisha kwa wakati katika mifuko ya hifadhi ya jamii michango ya wafanyakazi wake, hivyo kuwa sehemu ya kero ya wastaafu kutolipwa mafao yao kwa wakati.


Mdhibiti huyo anabainisha katika ripoti hiyo kuwa ucheleweshaji huo hauishii tu katika michango inayopaswa kuwasilishwa katika mifuko ya Hifadhi ya Jamii, bali pia makato yanayotakiwa kuwasilishwa katika Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya CAG, halmashauri za Jiji la Dodoma na Nzega Mjini, zinaongoza kwa kutowasilisha kwa wakati michango ya wafanyakazi wake.

Tunaunga mkono uamuzi wa serikali - hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya waajiri wa aina hii ili wazee wasiwe wanahangaika kupata mafao yao kisa mwajiri wake hakuwasilisha michango kwa wakati.

Mifuko hiyo imeanzishwa kisheria. Uwasilishaji michango kwa wakati ni agizo la kisheria, hivyo kutochukua hatua dhidi ya waajiri wanaovunja sheria ni kuungana nao kuvunja sheria za nchi. Shime, hatua zichukuliwe!

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Chonde chonde kumbukeni bima kuzilinda mali zenu



Na Sabato Kasika

**MARA** baada ya kuanzisha biashara, jambo la muhimu ambalo wataalam wa masuala ya bima wanawahimiza wawekezaji ni kujua namna bora ya kuilinda biashara yako isiharibike, kufa au kupotea.

Ufafanuzi wao ni kwamba, kuilinda dhidi ya wizi, majanga ya asili kama tetemeko na yale yasababishwayo na mwanadamu kama moto.

Na kwamba zipo njia zinazoweza kusaidia katika kuitunza biashara au mali ambayo wanaitaja kuwa ni bima.

Kuikatia bima kunatajwa kama mabadilishano ya fidia kati ya mmiliki wa biashara na kampuni ya bima katika kiwango fulani na kwa muhula au kipindi maalum kinachowekwa kwa mujibu wa sheria.

Ikumbukwe kulipia bima katika biashara, ni kuikinga isipate hasara endapo tatizo au janga lisilotarajiwa kama vile moto, wizi au majanga ya asili yatatokea vinapotokea, kwani wakala wa bima ataifidia hasara itakayotokea.

Ni wazi kwamba, bima ni njia bora itakayoiweka na kuikinga athari biashara na ndivyo ilivyotokea kwa baadhi ya wafanyabiashara wa Soko Kuu la Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Kwa wale wanaokumbuka, soko hilo liliungua na kusababisha mali za wafanyabiashara kuteketea, lakini 12 kati yao waliokuwa na bima mbalimbali, walilipwa fidia ya Shilingi milioni 438.4.

Benki na kampuni ya bima ilitoa malipo hayo, kwa waathirika hao, ambao walikiri walipata hasara na maumivu yao ya kuunguliwa angalau yalipozwa kwa malipo hayo ya haraka.

Hatua hiyo ya kukiri kupozwa machungu na bima, inapaswa kuwa chachu kwa wafanyabiashara wengine kuwa na bima za biashara, ili inapotokea ajali kama hiyo wawe na sehemu ya kukimbilia.

Kwa sababu kumekuwapo na wimbi la kuungua moto maduka makubwa sehemu mbalimbali nchini, jambo ambalo nadhani linatosha kuwashitua wafanyabiashara na kukata bima.

Kumekuwapo na uhamasishaji wa wafanyabiashara kukinga biashara dhidi ya hasara zitokanazo na majanga ya moto, wizi, uharibifu wa mali au akiba, hivyo ingekuwa ni vyema fursa hiyo isipite bure.

Ingawa ni muda umepita tangu tukio au sakata la Kariakoo kuteketea, lakini kwa jinsi lilivyotokea huku baadhi ya wafanyabiashara wakiambulia pa tupu na wengine kulipwa, fursa hiyo isingeachwa ipite bali inengwa ni nafasi kwa wenzao wasio na bima kutambua umuhimu wa kuwa nayo.

Hivyo, niwakumbushe wafanyabiashara kuwa tukio la moto Kariakoo ni nafasi ya kujifunza na kuchukua hatua ambazo zitakazowasaidia kufidiwa mali zao pale majanga yakiwamo ya moto yanapotokea.

Kimsingi, kufidiwa kunafanyika pale mfanyabiashara anapokuwa amekata bima, vinginevyo inakuwa ni vilio kwa wale watakaounguliwa mali zao bila kuwa na bima ambayo ingesaidia kuwapoza machungu.

Lakini kwa maneno mengine ninaweza kusema kuwa, kujihadhari na majenga ni kukata bima, kwani japokuwa mali zinaweza kuteketea kwa moto, lakini mhusika anaweza kufidiwa kuliko kubaki mtupu.

Mara kwa mara jamii imekuwa ikikumbushwa kuwa bima sio, kwa ajili ya pesa za mikopo, bali zipo za moto, magari, nyumba, afya, mali na nyinginezo, tunaona sasa ni wakati mwafaka wa kuchukua hatua.

Ninashauri hivyo, kwa sababu ya kuwapo kwa majanga ya moto maeneo mbalimbali nchini kuanzia katika masoko na maduka makubwa, huku mali za wafanyabiashara zikiteketea na wao kubaki bila kitu.

Kwa ujumla, matukio ya kuunguliwa mali, ninadhani yanatakiwa kuwa kama njia ya wafanyabiashara kujifunza jambo na kuchukua hatua zikiwamo za kukata bima, ili kuwa na uhakika wa kufidiwa.

Ni wazi kwamba, watu katika biashara, huwa wanatofautiana ukubwa wa mitaji, lakini inapotokea umewekeza fedha nyingi katika biashara fulani bila kuwa na bima, una hatari ya kuteketeza mali yake mwenyewe iwapo atakuwa ameshindwa kukata bima.

**SAFU**

## FIKRA MBADALA

# *Pongezi kwa TanTrade Maonesho ya Sabasaba*



**Pascal Mayalla**

MABORESHO ya Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam, maarufu Sabasaba, yanazidi kuwa bora mwaka hadi mwaka. Maboresho ya mwaka huu yametia fora.

Kwa ambao hamjatembelea maonesho hayo mwaka huu, njooni na mtakubaliana na mimi. Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Latifa Mohammed Khamis, anastahili apewe maua yake!

Wasomaji wangu, baada ya makala mfufulizo kuhusu ukodishwaji wa bandari yetu kwa Kampuni ya DPW, leo tupumzike na kuzungumza vitu vizuri kwa nchi yetu, tuzungumzie Maonesho ya Sabasaba.

Juzi tarehe 7 mwezi Julai ilikuwa ni Sikukuu ya Sabasaba. Wengi wa kizazi hiki hawajui hata chimbuko la sikukuu yenyewe. Sabasaba ni tarehe ya kuzaliwa kwa chama cha TANU. Kilizaliwa tarehe 7 mwezi Julai, 1954, hivyo ikafanywa ni sikukuu na siku ya mapumziko mpaka leo.

Baada ya vyama vya TANU na ASP kuungana kuzaliwa kwa CCM tarehe 5 Februari 1977, siku ya kuzaliwa CCM pia ilikuwa siku ya mapumziko. Baada ya nchi yetu kuanza mfumo wa vyama vingi, siku ya mapumziko ya kuzaliwa kwa CCM, ilifutwa lakini siku ya mapumziko ya kuzaliwa TANU yaani Sabasaba ilibaki na kubadilishwa jina na kuitwa sikukuu ya Sabasaba na kuendana na Maonesho ya Sabasaba.

Kwa vile mimi ni mwandishi wa habari, nina wajibu wa kuwafunza watu lugha yetu adhimu ya Kiswahili sanifu, wengi wakiyaita ni 'Maonyesho', lugha sanifu ni 'Maonesho' na sio 'Maonyesho'.

Mimi nilikuja jijini Dar es Salaam mwaka 1977, hivyo Sabasaba yangu ya kwanza ni ya mwaka 1978. Tangu hapo sijawahi kukosa Sabasaba hata moja mpaka leo.

Enzi zile Maonesho ya Sabasaba, siku yenyewe ya Sabasaba kwa vile ni siku ya mapumziko, ilikuwa ni siku ya familia nzima, hivyo huo 'mtiti wa foleni ya magari kufika viwanja vya Sabasaba ilikuwa shughuli.

Na baada ya kufika, mahali pa kuegesha magari ilikuwa shughuli nyingine, na ukikosa pa kuegesha ukaamua kuondoka, unakuta hakuna namna ya kuondoka tena, umeshakuwa 'blocked', hivyo lazima utasubiri tu.

Foleni ya kukata tiketi kuingia ilikuwa shughuli nyingine, lakini shughuli pevu ilikuwa ni humo ndani umati wa watu kuingia kwenye mabanda na vivutio ni foleni kila pahala!

Taasisi zote za mashirika ya umma zilikuwa zinaonesha shughuli zake, Shirika la Reli (TRC) likiweka reli kuuzunguka uwanja wote kwa kiberenge. Kulikuwa na bembea. Ilikuwa raha sana!

Enzi hizo, barabara zote za uwanja huo ni za vumbi, siku ya Sabasaba jioni watu wana vumbi hadi nywele na kope zinabadili rangi. Ili kupunguza vumbi, gari la maji lilimwaga maji barabara kuu. Na ikinyesha mvua, hilo tope lake, ni usipime!

Enzi hizo Sabasaba ilisimamiwa na Halmashauri ya Biashara ya Nje, BET chini ya Mbaruku Mwandoro (apumzike kwa amani), ikaja Sabasaba ya Emmanuel Buliki, ikaja ya Ramadhan Khalfani na ndipo ikabadili jina kuwa TanTrade, akaja Jacline Mneney Maleko, mabadiliko makubwa yakaanza, akaingia Balozi Edwin Rutageruka, mabadiliko yakaendelea na sasa yupo mwanamama mpole, muungwana na mtaratibu Latifah.

Maonesho ya Sabasaba ni makubwa. Kwa mara ya kwanza barabara zote za viwanjani zimepigwa lami, hakuna tena vumbi!

Hali ya mabanda ilikuwa ya kawaida sana vingi vikiwa vibanda vya muda tu, hadi sasa kuna mabanda ya kudumu, hadi yenye viyoyozi!

Washiriki wa Kitaifa wameongezeka, bidhaa zimekuwa bora zaidi, huku washiriki wa kimataifa wakiongezeka na mabanda yenye hadhi ya kimataifa, yakiongezeka, mfano mzuri ni banda la Brands of China.

Kiukweli kabisa TanTrade ya Latifah, inastahili pongezi za dhati, kwa mambo makubwa mazuri ya maonesho ya mwaka huu. Ile makala yangu, kupongeza Expo Dubai, niliuliza hivi Tanzania hatuwezi kufanya Expo Tanzania? Sasa inaanza kupata majibu, mambo yakiendelea hivi, huko tuendako, tunaweza kabisa kuwa na Dar es Salaam Expo.

Pamoja na pongezi zangu kwa TanTrade, kila kwenye mafanikio hapakosi changamoto, bado zipo changamoto hizi na zile za kuboresha zaidi, kwa vile hii ni makala ya kupongeza TanTrade kwa kuboresha maonesho hayo, changamoto nitaziweka kwanza kiporo.

Leo ninampa maua yake Mkurugenzi wa TanTrade, Latifah Mohamed Khamis, apewe maua yake! Tena si yeye peke yake, pia bodi nzima ya TanTrade, menejimenti na wafanyakazi wote wa TanTrade. Wanastahili kupewa maua yao!

Ninawatakie maonesho mema na wale ambao hamjakwenda kuyashuhudia, nendeni! Maonesho yanaendelea mpaka Alhamisi ya tarehe 13 ya mwezi huu.

**Paskali**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# *Tunyoe nywele, tufue nguo kuepuka chawa hawa!*



**Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)**

**Ukisikia watu wameanza kukuita majina ya wanyama kama fisi na kadhalika, hususan wale ambao ni wachafu, ujue wamekuchoka. Wachache wanaitwa simba kutokana na ujasiri wa mnyama husika.**

UKIAMKA asubuhi ukakutana na mtu akusalimu 'we mbwa hujambo?' Utamjibu au utakaa kimya huku ukiugulia hasira?

Ukiwa njiani mara mtu anakuita, 'we panya sijakuona muda ulikuwa safari au unaumwa?' Utamjibu nini?

Kuna bosi katika kampuni moja alikuwa na mazoea ya kumwita aliyekosea jambo kuwa, 'we kunguni wewe!' Sina uhakika aliyekuwa anaitwa hivyo alijisikiaje!

Lakini nina hakika mathalani mtu akikuita jina la mnyama au mdudu, lazima utakasirika, kwani si vyema binadamu kufananishwa na mnyama au mdudu.

Na hakika majina ya wanyama yamekuwa yakitumika kutukana. Mnakumbuka Iddi Amin Dadah wa Uganda na majeshi yake alipovamia ardhi ya Tanzania miaka ya sabini!

Hakika tulimpachika jina la joka na hatimaye nduli. Tulikaribia kumwita shetani, lakini kwa kuwa haonekani tukabaki kumwita joka na majina mengine machafu.

Ukisikia watu wameanza kukuita majina ya wanyama kama fisi na kadhalika, hususan wale ambao ni wachafu, ujue wamekuchoka. Wachache wanaitwa simba kutokana na ujasiri wa mnyama husika.

Inashangaza siku hizi watu wanajiita mende wengine chawa. Unasikia mtu anajiita chawa wa fulani na anaridhika kuitwa hivyo kwa kadamnasi.

Mimi chawa wa Mama au sisi chawa wa Mama. Hao ni wanawake na wanaume wanaojinasibisha kuwa karibu na Rais Samia Suluhu Hassan, hata kama yeye hawajui.

Yawezekana wana nia njema ya kutaka kuonesha kuwa wanamuunga mkono katika mambo anayoifanyia nchi, lakini yawezekana wakawa wamekosea kujitambulisha kwa jina hilo.

Wanajua kabisa nini asili ya mdudu chawa, tabia na maskani yake. Chawa ni mdudu mchafu anayeishi katika mazingira yenye uchafu.

Tukiwa shuleni, walimu walikuwa wakitutaka kunyoa nywele, kuchelewa hufuga chawa. Wakitutaka kufua nguo kuepuka chawa, kwa sababu nguo na nywele chafu ni makazi ya chawa.

Kwa maana hiyo basi, mtu anapojitambulisha kuwa chawa wa Mama, hujitambulisha kuwa mchafu na mmiliki wake pia ni mchafu, kwani ndiye maskani yake.

Wanamaanisha kuwa pengine nywele au nguo za Mama ni chafu kiasi cha kuwa makazi au maskani ya wadudu hao wachafu wasiopendwa katika mazingira safi.

Sina uhakika kama Mama anapenda kuhusishwa na chawa, ila tu watu wanatafuta kujikaribisha kwake na wakati mwingine kujiwekea uzio dhidi ya wengine kujisogeza.

Lakini nina uhakika kuwa Mama Samia ni wa kila Mtanzania kama ambavyo amekwishajitanabaisha akizungumza na wote tofauti na alivyokuwa mtangulizi wake, aliyeona wapinzani ni maadui wasiostahili maendeleo.

Tulipata kushuhudia katika kipindi cha utawala uliopita, ambapo kuliibuka watu wa aina ya chawa hawa wakijinasibu kuwa karibu na kiongozi aliyekuwapo na kuponda waliowaona kuwa hawana unasaba nao.

Huko kulikuwa ni kujitenga na kukaa mbali na wenzao na kuondokana na imani ya Watanzania waliyonayo kwa miaka mingi, ya umoja na mshikamano wao.

Watu wakitumia nafasi zao kujisogeza kwa viongozi kwa maslahi binafsi ya kutamani kuteuliwa au kuwa nafasi katika uongozi wa nchi au eneo kwa nia ile ile ya kujaza matumbo.

Ukiona mtu anaingia katika mkumbo wa kukubali kuitwa jina la mdudu mchafu kwa lengo la kimaslahi basi ni wa kumwepuka kama ukoma, kwani ana nia ovu ya kuvuruga umoja uliopo.

Watu hawa hujitokeza na kujisogeza mbele ya kiongozi wakijionesha kuwa ndio waaminifu kwake lakini kumbe wakimchimba na kumng'ong'a anapokwama. Hapo ndipo chawa humwachia maradhi mwenyeji wake.

Bila shaka Rais Samia kutokana na namna ya uongozi wake, anajua fika kuwa kuna chawa waaminifu na wasio waaminifu, na hivyo kuongoza kwa hekima na busara kama afanyavyo.

Ila jambo la msingi ni kuwaepuka chawa hawa na kujikita katika kuongoza Watanzania kwa dhamira na malengo mema ya kuwafikisha katika maendeleo ya uhakika.

Hivyo basi wanaojiita chawa tuwatambue kwa uchafu wao na kuwanyima makazi na mazalia, kwa maana ya kunyoa nywele na kufua nguo zetu, ili wasipate mazalia na kutusababishia maradhi.

Siku zote chawa ni mchafu na ataishi katika mazingira machafu, tusipowaepuka chawa tutavuna maradhi katika nchi yetu.

Tujikombe kwa kiasi na tutumie muda mwingi kumsaidia Rais Samia aendelee kutuongoza badala ya kujificha kwenye nywele na nguo chafu.

**Alamsiki!**

# NIC yawaita wakulima kupata huduma za bima

**Na Restuta James**

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC) limewataka wakulima wa mazao 10 kukata bima ya kujilinda dhidi ya ukame, mafuriko, magonjwa, wadudu wasiodhibitika au kutibika, vimbunga na mvua ya mawe, ili majanga hayo yatakapotokea wasitetereke kibiashara.

Mkurugenzi wa Masoko wa NIC, Karim Meshack, alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na wananchi waliotembelea banda la shirika hilo katika Maonesho ya Sabasaba yanayoendelea Dar es Salaam.

Alisema, wakulima wa mazao ya pamba, korosho, kahawa, tumbaku, maharage, mahindi, mpunga, shayiri, alizeti na chai, wako katika nafasi nzuri kupata bima.

"Hii bima inalenga kumrudisha mkulima kwenye hali yake kabla ya kupata hasara ya majanga yaliyokingwa, kupata mikopo yenye masharti nafuu toka katika taasisi za kifedha, kukuza uwekezaji na kumpa amani ya moyo," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mkulima atakayekata bima ya mazao, atalipwa fidia ya upungufu wa uzalishaji kwa kiwango kitakachofanyiwa tathmini baada ya majanga kutokea ambayo yatalipwa mwisho wa msimu wa kilimo.

Alisema katika kundi hilo, NIC inatoa bima mesto, ya hali ya hewa na ya maeneo.

Meshack alisema bidhaa nyingine ya NIC ni bima ya maisha inayoitwa beamlife, ambayo inampa mteja faida ya fedha yake anayokuwa amewekeza.

Alisema, mwananchi yeyote anaweza kujiunga na bima hiyo kwa kuwa inatoa nafasi ya kuchangia kidogokidogo kuanzia Sh. 5,000 na kwa mkupuo pia.

"Faida ya Beamlife ni uwekezaji unaoongeza ukwasi na fidia kutokana na msiba... inatoa mafao ya uwekezaji wa kampaundi na fidia kwa wanachama na wategemezi kwa wakati mmoja," alisema.

Meshack alisema bima hiyo inampa mteja nafasi ya kuendelea kupata faida kupitia michango yake hata pale anapositisha kuchangia kutokana na sababu mbalimbali.

"Mteja akisitisha kuchangia ataendelea kupata faida ya uwekezaji na akimaliza mkataba atalipwa jumla ya michango yake na faida inayotokana na uwekezaji wa riba," alifafanua.

Meshack aliongeza: "Kwenye beamlife hata ukilipwa rambirambi, bado mafao yako yanayotokana na uwekezaji yatakuwapo."

# Nape ajivunia kukua kwa TEHAMA

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia Habari, Nape Nnauye, amesema kukua kwa Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kunaifanya Tanzania kuingia katika mapinduzi ya kidigitali duniani ambayo ni chanzo cha maendeleo uchumi endelevu.

Amesema matarajio ya nchi ni kwamba, miaka michache ijayo, wafanya kampeni za kisiasa kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano ya hologramu ambayo huruhusu washiriki wa mikutano kuonana mubashara.

Nape, aliyasema hayo jana katika banda la Expo Village katika Maonesho ya Sabasaba yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere mkoani Dar es Salaam wakati wa mkutano wa TEHAMA kati ya wizara hiyo na taasisi zake.

"Huduma za kifedha kidigitali Tanzania zimekuwa imara na tukishirikiana na mtandao kuwa salama na unaolindwa na kuepukana na matapeli, utakuwa bora na huduma ya uhakika," alisema Nape.

Alisema mikakati ya kujenga uchumi wa kidigitali inahitajika, na miongoni mwake ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kutaka zipitiwe sera, ili kuifanya sekta hiyo kuwa bora.

"Rais (Samia) aliagiza kupitiwa kwa sera ili kulifanya eneo hili kuwa bora, eneo hili la TEHAMA, sheria za ovyo zifutwe, zinazohusu kukwamisha maendeleo.

"Sheria inatungwa ili zifanye kazi na si vinginevyo. Lazima sheria zetu na kanuni zetu zifanane na dunia inakokwenda ili kuwapo mikakati ya pamoja ya maendeleo.

"Ikiwezekana tufanye kampeni mtandaoni kwa hologram. Nifunge kampeni watu wakapige kura. Hata mahakamani hakimu asikilize mashauri na kesi iishe. Tukiwa na sera bora na miundombinu, tutakuwa na uchumi wa kidigitali imara," alisema.

Nape alitaka mamlaka hiyo ifanye maboresho ya maonesho kwa kuhakikisha kila mtaa na banda lina vibao kama vile vya anuani ya makazi ili kutoa maelekezo kwa wageni wanayoyatembelea. "Kazi uliyoifanya Mkurugenzi wa TanTrade, haijifichi, watu wamefurahi kwa kupata huduma," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Latifa Khamis, alisema maboresho ya maonesho hayo yametokana na ushirikiano baina ya mamlaka hiyo na taasisi tofauti, ikiwamo za mifumo ya TEHAMA.

"Tumefanya maboresho ya mifumo ya kifedha na tunatarajia kutumia zaidi cashless (kutembea bila fedha mkononi) na tunaahidi tutatumia huduma hii katika Sabasaba zijazo na tutazidi kufanya maboresho zaidi ya maonesho haya," alisema Latifa.



Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Habas (katikati), akiangalia Nyumba ya Kabila la Wazanaki katika viwanja vya maonesho ya 47 Sabasaba Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri aonya matumizi ramani zisizothibitishwa na wizara yake

**Na Anthony Ishengoma**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka watanzania kuhakikisha wanatumia ramani sahihi zinazotolewa na wizara yake ambazo zimethibitishwa na Mpima Ardhi Mkuu wa Serikali kutoka wizara yake.

Amesema kumekuwa na ramani alizoziita za ajabuajabu zinazouzwa mitaani ambazo hazijathibitishwa na Mkurugenzi Mkuu wa Upimaji na Ramani aliyeko Wizara ya Ardhi, hivyo kawataka watanzania wanapotaka kununua ramani inayoonesha mipaka na utawala maeneo sahihi ya kupata ramani hizo ni Wizara ya Ardhi.

Waziri huyo alisema hayo juzi katika Maonesho ya Sabasaba alipotembelea banda la wizara yake kujionea huduma zinazotolewa kwa wananchi wanaofika kupata huduma zinazopatikana katika sekta ya ardhi.

"Kumekuwa na ramani nyingi zinazouzwa lakini ukiangalia vipimo vyake au namna walivyotenga maeneo hayo ni tofauti na kumbukumbu zetu za upimaji ramani, hivyo watanzania tumieni fursa hii kama ukitaka kuchukua ramani ya eneo lako, basi fika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi upate ramani sahihi na iliyothibitishwa," alitoa angalizo.

Waziri Mabula aliitaka jamii kutambua kuwa wizara yake ndiyo sehemu pekee nchini ya kupata ramani na si vinginevyo.

Alisema, watanzania wengi wanatumia ramani zisizo sahihi na wala hawajui pa kwenda kuchukua ramani hizo.

Kiongozi huyo alitumia fursa hiyo kuwakumbusha wananchi ambao walikabidhiwa juzi hati zao kutolimbikiza kodi ya ardhi, akionya kuwa kulimbikiza kodi hiyo kunachangia wanachi wengi kushindwa kulipa kodi ya pango la Ardhi.

"Unaweza kukuta gharama ya kulipa ni ndogo lakini ukimaliza mwaka mmoja na mwingine bila kulipa kodi inakuwa kubwa, hivyo niombe ninyi mnaochukua hati leo (juzi) kuhakikisha mnalipa kodi ya ardhi kila mwaka.

"Haipendezi wewe leo unalipa mwaka ujao haulipi, unasubiri mwaka mwingine ukianza kulimbikiza kodi inakuwa ni shida," alisema.

Waziri Mabula pia, aliwakumbusha wananchi kuhusu msamaha wa riba ya kodi ya pango la ardhi uliotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan wa Julai 31, 2022 hadi Aprili 21 mwaka huu lakini watu hawakutumia fursa hiyo kulipa kodi ya pango ardhi ndiyo maana akaendelea kusisitiza umuhimu wa kulipa hiyo kwa kuwa fursa hiyo haijitokezi mara kwa mara.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inashiriki katika Maonesho ya Sabasaba yanayoendelea Dar es Salaam, kutoa huduma za hati, kutatua changamoto kwa wananchi, kutoa elimu kwa umma na kushirikiana na sekta binafsi kutoa huduma za ardhi kupitia maonesho hayo.

# MAISHA

JULAI 9, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*


Ukurasa 14




## TAMBI ZA MAYAI

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15






## KATUNIKA


Ukurasa 16




# KANUNI ZA KUJIPODOA

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | J | E | M | B | E |
| ■ | A | ■ | ■ | O | ■ |
| U | M | A | ■ | N | ■ |
| ■ | B | ■ | I | G | A |
| ■ | I | ■ | ■ | E | ■ |
| J | A | N | G | A | ■ |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

YAI, NAO, BAA, PUA, USIKU, IFUTE, YANGU, ILIPO, ASUBUHI, UCHACHU

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

HAYA WATOTO. NI WAKATI WA SOMO LA KIINGEREZA KUPITIA FUMBO LETU HILI; TAFUTA MAJINA YAFUATAYO **WINO, KALAMU, KITABU** NA **CHAKI** AMBAYO YAMEANDIKWA KWA LUGHA YA KIINGEREZA.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| C | C | P | E | N | B |
| H | A | X | B | U | U |
| A | W | Y | O | O | I |
| L | I | J | O | J | N |
| K | B | P | K | O | K |
| R | U | L | E | R | R |

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

BAADA YA JAMBAZI KUVAMIA KANISA

Jambazi mmoja aliingia kanisani na bunduki akapiga risasi juu ya bati akasema “asiyempenda YESU atoke nje” wakatoka wote isipokuwa mchungaji na wazee wawili.

Jambazi likamwambia mchungaji “unaweza kuendelea na ibada, nilikuwa nakuondolea wanafiki”, Mchungaji akasema “ungewaacha kwanza nichukue sadaka...!

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Ufanye nini unapoishi na mkwe muda mrefu?

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada yetu ya mama mkwe. Makala tatu hivi mfululizo zilipata wachangiaji mbalimbali wakikubaliana na yale yaliyochambuliwa, huku wengine wakijitolea mifano jinsi mada ilivyowafumbua macho.

"Anti Flora, nimesoma ushauri wako kwenye Nipashe, ni ukweli tu endelea kuwaeleza wengi wafunguke akili zao. Nimejaribu kumwelimisha mke wangu kuhusu kumpenda mama yangu tuishi kwa furaha hakunielewa. Lakini baada ya kusoma gazeti la Nipashe juzi, ameelewa sasa. Ubarikiwe. Joel Meeli wa Arusha".

Msomaji mwingine akasema katika ujumbe wake "kuna wakwe dada, wewe mwenyewe utasema basi! Mke wangu ana tatizo la kuharibika mimba. Nikaona ngoja nipate wazo kwa mama mkwe. Hilo jibu alilonipa mpaka leo sina hamu naye. Eti, "unashangaa watoto?".

Msomaji huyu alinisimulia kwa kirefu yale anayopitia. Kisa chake ninakiandaa nitakileta hapa siku chache zijazo. Hiyo ni mifano michache ya wasomaji wetu. Kabla sijakuletea msomaji wangu vituko vya mawifi, leo nimalizie kutaja sababu zitakazofanya uishi vizuri na mama mkwe.

Mara nyingi haishauriwi wakwe waishi na wanandoa wachanga (waliooana karibuni). Lakini katika utamaduni wa kiafrika yapo mambo hutokea ambayo yanalazimu kuishi na wakwe ama kwa muda au milele.

Hebu nikupitishe katika sababu chache kumfanya mkwe aishi na ninyi. Pale wanandoa wanapojaliwa kupata mtoto wa kwanza na wanahitaji msaada wa mtu mzima ili kuwapa maelekezo ya jinsi ya kumpa huduma mtoto.

Pale wazazi wa mwanaume wanapokuja kuishi ili kupata msaada wa matibabu au pale wazazi wanapozeeka na hawawezi kujihudumia wenyewe.

Lakini, kama mama mkwe ataendelea kuishi nyumbani kwako kwa muda usioeleweka, yapo mambo unayopaswa kufanya ili kuepuka migongano ambayo inaweza kutokea na kusababisha matatizo kwenye familia yenu.

Unatakiwa kumwomba Mungu aingilie kati na akupe hekima jinsi ya kuishi na kumpa huduma huyo mama mkwe. Uwe na hekima na umakini jinsi ya kumwingia wakati unapotaka kuongea naye. Mwandalie chakula chake mapema na usije ukampa kazi ya kusimamia jiko(hiyo ofisi ni yako uwapo nyumbani).

Usije ukagombana na mumeo mbele za macho yake au usije ukamsema mumeo kwake kwani atamwegemea mtoto wake. Usiwe mchoyo au mwenye matumizi mabaya ya fedha, tumia fedha zenu kwa heshima.

Hakikisha mama mkwe ana chumba chake kinachojitegemea, na unakitunza kwa kukisafisha, kutandika mashuka safi na kadhalika.

Usije ukampayukia unapoongea naye. Au usiongee naye kwa sauti kubwa kwani anaweza kuhisi kuwa una roho mbaya. Kuwa mwepesi kuomba msamaha kama umemkosea au hata kama unahisi haujamkosea.

Hata kama amekufanyia ubaya, mseme kwa mume wako, ila tumia lugha itakayomfanya mumeo asihisi kuwa unataka mama yake aondoke hapo nyumbani kwenu.

Kuwa karibu na mume wako na pia usimfanye mama mkwe ajisikie mpweke. Mshukuru mume wako mbele za mama mkwe pale anapofanya jambo jema kama kumnunulia mama yake zawadi. Hapo ili mama mkwe ajue kuwa unapenda kumpongeza mumeo.

Onesha heshima kwa mumeo mbele ya mama mkwe, naye atakuheshimu. Tafuta muda wa kujadiliana naye. Usimfanye kama mgeni, ni mama yako, mfanye ajisikie huru.

Kama hajasoma au hajawa na maarifa ya darasani kama uliyo nayo, usiongee lugha ya Kiingereza ukiwa naye. Zungumza lugha anayoielewa ili naye aelewe nini unachozungumza na awe sehemu ya maongezi yenu.

Kama lipo jambo la siri unataka kumwambia mumeo, subiri utamweleza mkiwa chumbani. Usimtawale mumeo, mpe nafasi ya kuongea na mama yake pia.

Mfanyie mama mkwe yale ambayo unapenda ufanyiwe siku za usoni. Usije ukajifanya unajua zaidi yake hata kama hajasoma.

Wazee wanajulikana kwa kuwaharibu, kuwadekeza wajukuu zao. Usije ukamwachia sehemu ya nidhamu ya watoto wako. Lakini usionyeshe kama unapingana naye katika uamuzi anaofanya juu ya watoto wako.

Kama unahitaji kumsahihisha, fanya hivyo kwa upendo. Tumia hekima kukataa mawazo mabaya ambayo anaweza kutoa. Usimkasirikie, mchukulie kama mama mazazi.

Anaweza akawa anapenda vyakula vya asili na kama hujui kuviandaa, mwombe akufundishe ili uwe unampikia. Mwombee sana unapokuwa naye!

***Wiki ijayo: Jinsi ya kuchukuliana na mawifi na mashemeji. Una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Mwigulu, TRA hamjakisikia kilio cha NGO?

RAIS wa kwanza mweusi wa Afrika ya Kusini, Hayati Nelson Mandela, aliwahi kusema "usinihukumu mimi kwa mafanikio yangu, nihukumu mimi ni mara ngapi nimeanguka na kunyanyuka tena."

Nimejikuta nikisukumwa na ushawishi wa kuanza na nukuu hiyo ili kuijenga hoja yangu katika msingi ambao utakuwa na mwendelezo siku zijazo.

Jamii iliyostaarabika duniani kote inajua asasi za kiraia au mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) ni mkono wa pili wa serikali.

Kwamba kila wanachokifanya, ni kile ambacho serikali inapaswa kukifanya kutoa huduma kwa watu wake. Na ndiyo ukweli ulivyo!

Lakini sera na taratibu zinazosimamia utozaji kodi kwa asasi za kiraia, bado si rafiki kwa wanaoanzisha na kuendesha mashirika hayo yasiyo ya kiserikali.

Hakuna shaka kwamba asasi za kiraia zinawajibika kulipa kodi na kuwasilisha ritani kwa mujibu wa Sheria Na. 24 ya Mwaka 2002.

Kiuhalisia, ritani ya kodi ni hati inayowasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambayo inaonyesha mapato, gharama na taarifa nyingine zinazohusiana na mwenendo wa shughuli zake za kiuchumi kama inavyotakiwa kisheria.

Hivi sasa ritani ya kodi zinahitajika kuwasilishwa kwa njia ya kielektroniki (e filling) kwa madhumuni ya urahisi.

Ni kweli kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali yamesamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye uingizaji au/ununuzi wa bidhaa au huduma kwa shirika lenye makubaliano na serikali kwa ajili ya mradi unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali.

Yote hayo yanafanyika ikiwa makubaliano hayo yameainishwa kuwa msamaha wa kodi hiyo kwa bidhaa au huduma.

Wiki hii kuliripotiwa kilio cha kodi ya mwaka ya asilimia 30 inayotokana na mavuno ya mapato ya NGO, kwamba inawaumiza kwa vile wao hawafanyi biashara zaidi ya kutoa huduma.

Mratibu wa Taifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Wakili Onesmo Ole Ngurumwa, amenukuliwa akisema ziko kodi za kawaida ambazo wanaweza wakalipa, lakini zingine ambazo wanatozwa, akitolea mfano kodi ya mwaka ya asilimia 30 ya mapato. Wao hawana mapato.

Ole Ngurumwa anasema "sisi tuna ruzuku, na ruzuku siyo ya mtu binafsi ni ya kutoa huduma. Sasa ruzuku yangu ambayo inatumika mwaka kesho, ukiipiga asilimia 30 maana yake umeenda kutumia fedha za miradi.

"...Ndiyo maana tumeona tukae vizuri na ndugu zetu wa TRA (Mamlaka ya Mapato) pamoja na serikali ili tuweze kuona ni namna gani tutaboresha sheria za kodi".

Maana yake ni kwamba, kilio hiki cha asasi za kiraia kimezagaa kila kona ya nchi. Wanalia! Na ombi lao kubwa ni kupata misamaha ya kodi hiyo inayolalamikiwa.

Msajili Msaidizi wa NGO's Mkoa wa Kilimanjaro, Jesca Nyaki, amenukuliwa akisema mkoa huo wenye jumla ya mashirika yasiyo ya kiserikali 443, yaliyosajiliwa chini ya sheria ya uratibu wa sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali Na. 24 ya Mwaka 2002, ni 110 peke yake ambayo yameweza kuwasilisha taarifa zao na miradi wanayoitekeleza, lakini 333 yameficha taarifa zao na hawajulikani wanafanya nini.

Mashirika yaliyojisalimisha mwaka 2022, ni yale yanayotekeleza shughuli mbalimbali zikiwamo shughuli za afya, elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia na elimu ya ujasiriamali.

Mengine ni yale ya ukuzaji wa uchumi, utunzaji wa mazingira na wako wadau ambao wanatoa huduma za msaada wa kisheria na kusaidia watoto wanaoishi mazingira magumu kwa kuanzisha vituo vya kulea watoto.

Tukiangalia kwa mwaka 2022, yametekeleza shughuli mbalimbali ambazo zina takribani ya thamani ya Sh. bilioni 6.1. Hawa wapewe maua yao!

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kwa mamlaka uliyonayo na nafasi aliyopewa ya kumshauri Rais katika masuala ya kodi, atazame upya tozo ya kodi ya asilimia 30 wanayotozwa NGO.


***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***


# HARUSI






Je, ungependa baada ya harusi kufurahia fungate yenu kwa kupiga picha nzuri? Hizi ni baadhi ya picha zenye mikao tofauti mnayoweza kupiga mkiwa sehemu ya mapumziko. PICHA: PINTEREST









# MITINDO

Na Mary Geofrey





## JIPE JOTO NA MITANDIO


MITANDIO sio vazi la wanawake pekee, hata wanaume wanalitumia wakiwa katika mazingira tofauti yanayowazunguka.

Katika mazingira ya baridi vazi la mtandio linafaa zaidi kwa wanaume katika kuuweka mwili sawa na kuepuka kero ya kipupwe.

Ikiwa unapenda kuvaa mavazi anuwai wakati unapoenda kazini au kukaa na marafiki, ni vazi gani zuri zaidi ya kitambaa chembamba kinachonakshi vyema mavazi yako ya kila siku, huku ukijilinda na baridi.

Kuna mitindo ya aina nyingi ya kutumia mitandao, lakini yote inamaanisha jambo moja tu, ni kukupatia joto na pia kukupa mwonekano nadhifu mbele ya watu.

Ikiwa umevaa suruali na shati, jeans na fulana na koti au mtindo usio rasmi, kwa hali yoyote, unaweza kuweka kichwa na shingo yako katika hali ya joto kwa kutumia mitandio yenye vifuniko.





UREMBO

Na Mary Geofrey

# KANUNI ZA KUJIPODOA



VIPODOZI ni urembo unaopendwa na wanawake wengi kwa lengo la kuongeza uzuri na kubadili mwonekano.

kwa wale wanaopenda kujiremba wenyewe nyumbani kuna mambo muhimu tunakumbushana ambayo ni ya kuzingatia kabla hujapaka vipodozi yaani 'make-up' yako.

Jambo kubwa kabisa tafuta vipodozi vinavyoendana na ngozi yako usipake au kununua kwa kufuata mkumbo hapana.

Kila mtu ana rangi yake ya ngozi na mfano poda zimetengenezwa na aina mbalimbali za rangi.


Hivyo, inakupasa kufanya utafiti ili kubaini ni make-up ipi sahihi na haina madhara katika ngozi yako.

Watu wenye ngozi za mafuta wanashauriwa kupaka poda au ungaunga kwani cream inaweza kuziba vitundu vya hewa katika ngozi ya uso, hatimaye kusababisha chunusi kuota.

Wale walio na ngozi kavu mfahamu kuwa, make-up ya cream haina uwezo wa kukaa muda mrefu katika ngozi, hivyo ikiwa unahitaji iendelee kuonekana kwa muda usiopungua saa nane ni vyema ukapaka make-up ya poda iliyozeoleka na wengi.

Jambo jingine la kutilia msisitizo ni namna ya kupaka aina zote mbili za make up, inashauriwa make-up ya poda au unga ipakwe kwa brashi zake maalumu, siyo mikono wala kitambaa chochote ambacho hakijawekwa mahususi kwa kazi hiyo.

Ila kwa upande wa make-up ya cream au majimaji, inapaswa kupakwa kwa mikono na kusambazwa katika uso wote, ili kuwe na ulinganifu katika eneo hili linalokusudiwa.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Tambi za mayai

TAMBI ni chakula kizuri na rahisi kupika. Kutoka kwenye tambi tunapata madini na virutubisho mbalimbali kama protini na carbohydrate ambavyo vinatusaidia katika kujenga mwili.

Tujifunze pamoja namna tunaweza kupika tambi kwa muda mfupi na chakula kitamu sana.

Washa jiko chemsha maji kisha yatie chumvi na mafuta kidogo.

Weka tambi kwenye maji ya moto mpaka uhakikishe zimeiva kisha zichuje.

Chukua chombo chako chote iwe bakuli au kikombe piga mayai uyaweke pembeni.

Bandika sufuria jikoni weka mafuta kisha kitunguu maji, kitunguu saumu, pilipili hoho, karoti na curry powder kaanga kwa pamoja ila zisiive sana.

Ongeza tambi zako geuza zichanganyikane na zile mboga karoti, pilipili hoho na vingine.

Weka mayai kwenye tambi kisha koroga haraka haraka hadi mayai yaive. Tafadhari usiache kukoroga mpaka uhakikishe tambi zako zimekua kavu na mayai yameiva.

Na hapo chakula chako kitakua tayari ushindwe tu wewe kujiramba

Jilambe tambi zako kwa kunywa na juisi, chai, soda na maziwa.





MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Sinki zuri linapamba Chumba cha chakula

**Na Restuta James**

SINKI la kunawia mikono linatajwa kuwa sehemu ya pambo katika eneo la kulia chakula. Hii ni kutokana na mwonekano na muundo wake.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Winnie Joseph, ameiambia NIPASHE katika mahojiano maalumu kwamba kumekuwa na miundo mipya ya kuvutia inayoendelea kuvumbuliwa na wana teknolojia.

Anasema katika sehemu ya chakula, imekuja miundo mipya kuanzia kwenye ramani ya ujenzi wa nyumba hadi nakshi zinazokamilisha eneo hilo.

Anasema moja ya pambo linaloongeza thamani na mwonekano wa eneo hilo ni sinki la kunawia mikono.

"Wavumbuzi wamekuja na design (muundo), mpya wa kisasa ambao unaleta uhalisia (natural), ndani ya nyumba. Sinki la kunawia la jiwe lililopolishiwa vizuri kama unavyoona," anasema Winnie akionesha baadhi ya masinki hayo.

Anasema kitu pekee kinachovutia kwenye muundo huo ni utulivu (calmness), unaoletwa na sinki hilo.

Winnie anasema masinki hayo yanapatikana kwa rangi tofauti tofauti ikiwamo nyeusi, kahawia na kijivu.

Hata hivyo, anasema muundo huo haujafuta yale ya udongo ambayo yanatumika hivi sasa kwani bado kuna watu wanaopendelea aina hiyo.

NIPASHE ambayo imetembelea maduka tofauti jijini Dar es Salaama, imebaini kuwa 'mchawi' wa aina hiyo mpya ya sinki ni bei kwani ni kubwa ikilinganishwa na ya udongo yaliyozoeleka.





# Huisha nyumba uifurahie

WENGI wetu tunapenda ndani ya nyumba zetu kuwe na mvuto wa kuridhisha nafsi zetu.

Pamoja na kupenda huko, tumekuwa tunashindwa kuziridhisha nafsi hasa kutokana na kukosa kipato cha kutuwezesha kutengeneza nyumba zetu kama nafsi inavyopenda.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Lucas Kwambikwa, anasema zipo njia mbalimbali za kufikia angalau kwa kiwango fulani ambacho kinaweza kuridhisha nafsi kwa kuboresha nyumba yako ikawa na mvuto bila kutumia gharama kubwa.

Lucas anasema endapo nyumba yako imechakaa na haufurahishwi na mwonekano wake, unaweza kufumua rangi yake na kupaka upya na inaweza kuwa ileile au ukabadilisha nyingine mradi uwe umeridhika nayo ili kuipa mwonekano mpya.

Pia, anasema kubadilisha samani za ndani nayo inachangia kuupa mwonekano mpya nyumba yako, kwamba hata kama huna ya kuweka mpya, unaweza



kuzifanyia ukarabati mdogo ikiwamo kubadili kitambaa kama ni za kukalia sebuleni.

Mbali na samani, mapambo nayo yatakupa mwonekano mpya, kama uliweka na yana muda mrefu yamechakaa, weka mengine mapya.

Anasema ni muhimu kuwa na picha yako kichwani ya namna unavyotamani kubadili nyumba yako ili kila unachofanya marekebisho kiendane na matakwa yako.

Lucas anashauri kuondoa ndani ya nyumba vitu ambavyo havitumiki ili kuacha nyumba kuwa hewa ya kutosha na kukupa kufurahia kukaa muda mwingi bila kuchoka.


"Kwa mfano, badala ya kuweka vitu vingi ukutani, ukatafuta picha moja kubwa ya mvuto na kuibandika, hiyo haitamchosha mtu kuitazama."

Anashauri kuepuka kununua vitu vingi na kuviweka ndani ya nyumba kabla ya kufahamu matumizi yake na ni vyema kuhakikisha kwamba kila kitu kinachowekwa ndani ni kile kinachotumika.

Anataja baadhi ya vitu vingine vya msingi vya kuzingatia unaporudisha mwonekano wa nyumba yako kuwa ni pamoja na pazia au zuria. Kwamba wakati wa kuviweka ni muhimu kuhakikisha rangi zake ni zile zinazoshabihiana na vitu vilivyo ndani ya nyumba.

"Nyumba ni ubunifu, ukizingatia hili utafurahia nyumba yako na utapenda kukaa humo bila kuchoka," anasisitiza.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
DOKTA FARAGHA YANGU NI KWAMBA KWA NINI NACHOMOKA SANA NA VIDENTI LAKINI TUKIFIKA KULE SHUGHULI SINA?
MKEO ATAKUWA KAKUWAHI KWA MTAALAM UKIWEZA NENDA POLISI
NDUGU ZANGU NAOMBENI MNIAZIME MASIKIO YENU
OHOOO! KUNA MWENZAKO ALIAZIMWA LAKINI HAIKUJULIKANA ALIPOSHUKIA!
ALIYEKUTUMA VIUNGO HIVYO KAMWAMBIE WENYEWE WAMEKATAA
ANAWAZIMU NA MWENZAKE ALIYEMTUMA
ETI KUTELEZA SI 'KUBWAGIKA' NANI KASEMA?
TOKA NIISHI NA WEWE PESA SIPELEKI BENKI NARUDI NAZO ZOTE LAKINI SIZIONI!
NAE NAWE USIWAZE UJINGA, EBU NAMBIE "UTAKULA NDIO UOGE AU UTAKOGA NDIO ULE?"
TOKA DAR NIMEHAMI-SHIWA HUKU TANGA KIKAZI NILIGOMA MIE!
WOTE TUNAFURAHA LAKINI MWENZETU SURA IMEKUNJANA!
SIO SURA TU HATA ROHO NI HIVYO HIVYO NISHUSHENI JAMANI MIE SIWEZI!
ALIYEBUNI MADENI YA KAUSHA DAMU NAMSALIMU SHIKAMOO SANA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...POTEZA KAZI UJUE MIKAO YA BAO KIJIWENI

# Rais Zelensky atembelea kisiwa cha nyoka

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amechapisha video yake akitembelea katika kisiwa ambacho kilitumika kama ishara ya upinzani wa nchi yake dhidi ya Russia.

Kiongozi huyo amekanyaga ardhi ya kisiwa hicho maarufu kama kisiwa cha nyoka baada ya siku 500 tangu kuanza kwa vita.

Mwanzoni mwa vita, askari wa Ukraine waliokuwa Kisiwa hicho walikaidi amri kutoka kwa meli ya kivita ya Russia ya kujisalimisha.

Kisiwa hicho kilichopo kwenye Bahari Nyeusi kilitekwa na Russia, lakini baadaye kikarudishwa kwa Ukraine.

Katika video hiyo alionekana Rais Volodymyr akiita neo hilo kuwa mahali pa ushindi na hakitaweza kutekwa tena.

Kisiwa cha Nyoka ni muhimu kimkakati katika Vita vya Ukraine, nchi zote mbili zimekuwa ziking'ang'ana kukidhibiti. Katika video ambayo haikuonyeshwa tarehe iliyochukuliwa, iliyotumwa kwenye Telegram, kiongozi huyo alielezea kama dhibitisho kwamba Ukraine itarudisha kila inchi ya eneo lake lililochukuliwa na Russia tangu vita vilipoanza tarehe 24 Februari 2022.

"Ninataka kushukuru kutoka hapa, kutoka mahali hapa pa ushindi, kila mmoja wa askari wetu kwa siku hizi 500," alisema Zelensky kwenye video hiyo ambayo alionyeshwa akiwasili kisiwani kwa mashua na kuacha maua kwenye eneo la kumbukumbu. Wakati huo huo, jumla ya watoto 494 wameripotiwa kuuawa hadi sasa katika vita inayoendelelea, na zaidi ya watoto 1,050 walijeruhiwa.

Kulingana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Ukraine, watoto wengi waliathirika kutoka mikoa ya Donetsk, Kharkiv, Kyiv, Kherson, Zaporozhye, Mykolaiv, Dnepropetrovsk, Chernihiv na Lugansk.

Hata hivyo, takwimu hizi sio za mwisho, kwani inatokana na watoto ambao majina yao yalithibitishwa na serikali.

Takwimu za Umoja wa Mataifa inaeleza zaidi ya watoto 500 walikufa katika siku 500 za vita. Idadi ya jumla ya raia nchini Ukraine ambao wamekufa tangu mwanzo wa vita, tangu Februari 24, 2022, imepita watu 9000.Umoja wa Mataifa pia unafafanua kuwa kuna watu wengi zaidi waliofariki na kujeruhiwa, takwimu zilizotolewa zimeandikwa na kuthibitishwa wahanga wa vita hivyo.

**BBC**



Watu wakiwa wamepakiwa katika mkokoteni unaokokotwa na farasi kuvuka eneo lililofurika maji baada ya mvua kubwa kunyesha nchiniPakistani jana. **PICHA: EPA-EFE**

# Ubaguzi yaiangusha serikali Uholanzi

**AMSTERDAM**, UHOLANZI

WAZIRUI Mkuu wa Uholanzi Mark Rutte, ametangaza kujiuzulu usiku wa kuamkia jana baada ya kuanguka kwa serikali yake.

Rutte alisema tofauti zilizojitokeza kuhusu sera hiyo baina ya vyama washirika haziwezi kurekebishwa na kwamba uamuzi wa kuivunja serikali ulikuwa wa lazima.

Jana HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/mark-rutte-ashinda-uchaguzi-mkuu-uholanzi/a-37960519" Rutte alipangiwa kuwa na mkutano na Mfalme WillemAlexander kumwarifu rasmi uamuzi wake wa kujiuzulu na inatarajiwa uchaguzi mpya utaandaliwa mwezi Novemba.

Chanzo cha mvutano ni pendekezo la chama cha Rutte cha VVD kinachoegemea siasa za mrengo wa kulia la kutaka kuzuia wahamiaji walio nchini Uholanzi kujiunga na familia zao. Pendekezo hilo linapingwa vikali na chama cha kihafidhi na cha Christian Union kinachotaka uwepo uwezekano wa kuwaruhusu watoto wa wakimbizi wa vita kujiunga na wazazi wao nchini Uholanzi.

**DW**

# Saba wauawa kwenye ghasia India

**BENGAL,** INDIA

WATU saba wameuwawa na wengine kadhaa wamejeruhiwa nchini India baada ya kuzuka fujo wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa katika jimbo la Bengal Magharibi.

Hayo yameelezwa na jeshi la polisi katika jimbo hilo , ambalo linafanya uchaguzi wenye ushindani mkali wa kuwapata viongozi wa manispaa.

Zaidi ya wagombea 200, 000 wanawania nafasi hizo katika jimbo hilo lenye wakazi milioni 104. Mikanda ya video ilionesha wafanyakazi wa vyama hasimu wakizunguka mitaani wakiwa wamebeba bakora na masanduku ya kura waliyokwapua vituoni na katika maeneo mengine baada ya moto kuwashwa nje ya vituo vya kupiga kura.

Uhasama umeongezeka miaka ya hivi karibuni baina ya wafuasi wa chama cha Trinamool Congress kinachotawala Jimbo la Bengal Magharibi tangu mwaka 2011, dhidi ya wale wa chama cha waziri mkuu wa India, Narendra Modi cha BJP kinachonuwia kujiongezea umaarufu kwenye jimbo hilo.

**DW**

# Sall akaribisha Afrika kujiunga G20

**PARIS,** UFARANSA

RAIS wa Senegal Macky Sall, amesema ana matumaini kuwa mpango wa kuupatia Umoja wa Afrika kiti cha kudumu ndani ya kundi la mataifa ya G20 utakamilika wakati wa mkutano wa kundi hilo mwaka huu.

Akihutubia kwa njia ya mtandao mkutano wa masuala ya uchumi unaofanyika kwenye mji wa kusini mwa Ufaransa wa Aix-en-Provence, Sall alisema kuukaribisha Umoja wa Afrika ndani ya kundi la G20 utakuwa uamuzi wa kutenda haki iliyocheleweshwa.

Aliwambia wajumbe wanaoshiriki mkutano huo kuwa ameridhishwa na hatua inayopigwa kuelekea kuridhia Umoja wa Afrika kujiunga na kundi la G20 akikumbusha kuwa kwa jumla bara hilo linashika nafasi ya nane kwa thamani ya pato ghafi duniani.

Afrika Kusini ndiyo nchi pekee ya Afrika iliyo mwanachama wa HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/maoni-mkutano-wa-g20-waonyesha-kuwa-wakati-wa-nchi-zinazoinukia-umewadia/a-63787816" kundi la G20 linaloyaleta pamoja mataifa 19 tajiri na yale yanayoinukia pamoja na Umoja wa Ulaya.

**DW**

# Marekani yateketeza silaha za sumu

**WASHINGTON, MAREKANI**

Rais wa Marekani Joe Biden ametangaza kuwa nchi yake imeteketeza shehena ya mwisho ya silaha zake za kemikali.

Hatua hiyo ilisifiwa kuwa ya mafanikio makubwa kuelekea dhamira ya kuondoa silaha za aina hiyo ulimwenguni kote.

Tangazo la Biden limefuatia ukamilishaji wa kazi ya karibu miaka minne iliyokuwa ikifanywa kwenye kituo kimoja cha kijeshi huko Kentucky ya kuteketeza kiasi tani 500 za silaha za sumu ambazo ndiyo ilikuwa akiba ya mwisho ya silaha hizo nchini Marekani.

Rais Biden alisema anaona fahari kuwa Marekani imekamilisha kazi hiyo ya kuondoa kutoka uso wa dunia shehena ya silaha zinazofahamika kuwa na uwezo wa kuangamiza idadi kubwa ya watu.

Silaha za kemikali zinazojumuisha gesi za sumu na viambata vingine hatari zilipigwa marufuku duniani chini ya mkataba wa mwaka 1993 .

Tangu wakati huo HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/opcw-yakabidhiwa-tuzo-ya-nobel/a-17282510" shirika la kimataifa la kuzuia silaha za kemikali duniani limefanya kazi ya kusimamia uteketezaji wa silaha hizo kote ulimwenguni.

**DW**

MAKALA

# KUWA MSEMAJI WA TAASISI NI TAALUMA



Na Magabilo Masambu

**Hivi karibuni kumejitokeza tabia ya watu wanaosimama kuwa wasemaji wa taasisi, ambao kimsingi si wasemaji wenye taaluma ya taasisi hizo. Tabia hii ilianza kujitokeza zaidi katika hii miaka ya kuanzia 2016 mpaka sasa.**

UTAMADUNI na utaratibu wa nani aseme nini kwa niaba ya nani na wakati gani umekuwapo miaka mingi. Upo kila mahali duniani.

Hapa Afrika hata katika ngazi ya familia si kila mtu anaweza kuwa msemaji na kutoa chochote bila rukhsa ya fulani.

Tukiwa wadogo tulikuwa tunafundishwa aina fulani ya vitu tunavyopaswa kutoa, ikiwa mtu amekuja na shida na baadhi ya vitu hatukupewa rukhsa kabisa hata kama viko ndani tunaviona, tulisema ama havipo au mwenyewe hayupo.

Kwa baadhi ya jamii zetu, kwenye koo zao upo uongozi wa familia au ukoo. Inapotokea kuna jambo lolote la ukoo au familia hutakiwi kuwa msemaji wa jambo hilo mpaka ama uwe na rukhsa ya mwenye kulisema au yeye mwenyewe. Hii yote ilikuwa ni kulinda heshima ya familia au ukoo huo, kwa sababu aliyekabidhiwa mamlaka ya kuwa msemaji kabla ya kusema lazima awe amezungumza na watu wazima kwenye familia au ukoo huo na hivyo akijitokeza kuzungumza kila mtu anajua, huo ndiyo msimamo wa familia au ukoo na kwamba si maoni ya msemaji.

Kwa upande wa jamii, anaweza kujitokeza yeyote au kikundi kuisema familia fulani lakini katika familia hiyo hawezi kujitokeza yeyote kuzungumza kama ni jambo zito lenye kuhitaji uamzi mazito.

Hili linakwenda sambamba na watoto kupigwa marufuku kuingilia mazungumzo ya watu wazima. Yaani pengine baba yako anazungumza na mgeni na ni mtu mzima mwenzake, ni marufuku kwa mtoto kuanza kuchangia mada, siku hizi utafatibu huo umeanza kupotea. Siku hizi unakuta wazazi wanazungumza, mtoto naye humohumo, eti tunaambiwa 'tunakwenda na wakati' na kwamba ule utaratibu wa zamani ni unyanyasaji.

Hivi karibuni kumejitokeza tabia ya watu wanaosimama kuwa wasemaji wa taasisi, ambao kimsingi si wasemaji wenye taaluma ya taasisi hizo. Tabia hii ilianza kujitokeza zaidi katika hii miaka ya kuanzia 2016 mpaka sasa.

Ni kweli kwamba katiba yetu ya nchi inatoa nafasi ya sisi watanzania kuwa na uhuru wa maoni, lakini linapokuja suala la kuisemea taasisi ni muhimu wenye taaluma na haki hiyo kwa mujibu wa sheria zetu, wawe wasemaji kwa niaba ya taasisi hizo.

Kwa haraka inaweza kuonekana kwamba ni watetezi wa taasisi husika, lakini kwa sababu kuwa msemaji ni taaluma na inasomewa miaka mitatu na zaidi, ni muhimu taaluma ikatumika, kuliko kuwa na watu wenye uzoefu wa kuzungumza lakini si uzoefu wa kuzungumzia taasisi.

Hatari yake kubwa ni kwamba, kila watakachokizungumza wametumwa na taasisi, wakati mwingine kumbe hawatumwi, wanajituma na katika kujituma wanaweza kuonekana kwamba, wana nia njema kumbe nia waliyonayo ni kutafuta kutimiza malengo yao binafsi. Ndiyo maana leo wanayemsemea akiondoka kwenye nafasi watu walewale wataanza kumsema vibaya.

Wasemaji wa taasisi wapate na elimu juu ya misingi ya kuwasilisha hayo masuala, kwa kuwa lolote watakalolitoa litatafsiriwa kwamba wameagizwa na taasisi hata wakijitetea kwamba hawakutumwa, watu wataendelea kuamini kwamba walitumwa.

Haya masuala ya wasemaji wa taasisi za umma huko nyuma hayakuwapo, si kwamba matatizo hayakuwapo yalikuwapo, lakini siku hizi kila mmoja ni msemaji na mtetezi, inakuwa kama baadhi ya familia ambazo kwa kweli zimeangukia katika janga la kushindwa malezi ya watoto wao.

Mtoto kachelewa kurudi nyumbani baba anamwita na kumuuliza "kwanini umechelewa kurudi nyumbani?" Kabla mtoto hajajibu mama keshaingilia "kwani kuna shida gani? Mwache mtoto". Mtoto hajafua nguo, mama "kwanini hujafua nguo zako? Baba "mwache, dada atamfulia". Kuna familia hapo? Mwisho wa siku, mnakuwa na familia ya ovyo ambayo kila mtu anatafuta kuonekana mwema kwa watoto kwa kuwa msemaji wao, mwisho wa siku malezi ya watoto yanakuwa magumu.

Tukiwa na vitengo kisha tukashindwa kuviamini kwamba vinafanya kazi kwa niaba yetu na kwamba vinafanya kwa ufanisi na havihitaji msaada wa wasemaji, tutazua matatizo mengi yasiyotarajiwa na mwisho wa siku tunaishia kuwapa lawama watu wengine wasiohusika.

Huko nyuma pamoja na kwamba hapakuwa na taaluma ya darasani, wasemaji walizungumza kwa maelekezo. Hiyo ndiyo taaluma yenyewe.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mke anadai talaka, mume kashindwa kudai mahari yake



Na Adam Fungamwango

**Wanawake wengine walikuwa wanaogopa kurudi kwao kwa sababu za utamaduni uliojengeka hasa wa Waafrika kuwa ni aibu sana kwa mke kuachwa au kuonekana kurudi nyumbani kwao. Inaonekana kama ndoa imemshinda, hakufundwa vizuri kumlea mume kiasi kwamba amerudishwa nyumbani, hajui kupika, au amefanya jambo lolote la aibu lililofanywa kurudi kwao.**

MAPENZI hayajawahi kumuacha mtu salama na kwa bahati nzuri au mbaya si kwa tajiri au masikini.

Tatizo la mapenzi ni kwamba yanaweza kukutesa hata kama ukiwa na pesa nyingi, cheo, mamlaka, umaarufu, tajiri hata mfalme.

Watoto wa mjini wanasema hayana 'fomula', kwa sababu wakati wenye nazo wanateswa na mapenzi, ambaye hana kitu, lofa kabisa anaweza kuwa kuwa yeye anaburudika tu, hana wasiwasi wowote.

Hata hivyo, ni kwa muda tu kwa sababu mapenzi siku zote hayana uadui wa kudumu wala urafiki wa kudumu, yapo kwa yoyote yule, masikini leo atafurahia mapenzi kesho atalia, tajiri leo atalia lakini kesho atafurahi.

Usidhani pesa ndiyo itakufanya uwe na penzi la amani na utulivu moja kwa moja, au masikini asiwe kabisa na mapenzi au asiweze kufurahia.

Tukitoka huko, tunaangalia utofauti wa ndoa za zamani na za sasa. Kuna utofauti mkubwa kwa kila kitu. Kinamama wa zamani walikuwa hadi kuja kuachika nanga inapaa.

Labda mwanaume mwenyewe aamue kumuacha kwa kumpa talaka, lakini wao walikuwa wagumu sana kuondoka kwenye ndoa zao hata kama wananyanyaswa, kupigwa na ukatili mwingi waliokuwa wanafanyiwa.

"Ningekuwa pekee yangu bila shaka ningejinyonga, lakini moyo wangu wote kwa watoto." Ni sehemu na maneno kwenye wimbo wa 'Jiko Limenuna' wa Vijana Jazz Band mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Mashairi hayo yanaonyesha uhalisia na wanawake wa zamani jinsi walivyokuwa wakizitazama ndoa zao.

Mama anakubali kunyanyasika kwa sababu anaona akiondoka kurudi kwao, anaweza kuacha watoto, na kwa bahati mbaya wakipata mama mwingine mbaya, watasema. Anaamua kukomaa na kuvumilia mateso yote kwa kuwalinda watoto wake.

Wanawake wengine walikuwa wanaogopa kurudi kwao kwa sababu za utamaduni uliojengeka hasa wa Waafrika kuwa ni aibu sana kwa mke kuachwa au kuonekana kurudi nyumbani kwao.

Inaonekana kama ndoa imemshinda, hakufundwa vizuri kumlea mume kiasi kwamba amerudishwa nyumbani, hajui kupika, au amefanya jambo lolote la aibu lililofanywa kurudi kwao.

Wazazi nao walikuwa hawakubali kirahisi binti yao kurudi nyumbani kwa sababu yoyote ile ambayo kwao haiingii akilini.

Kwao ni aibu binti kurudi nyumbani, kwani wataonekana ameshindwa kumfunda.

"Mwanangu rudi kwa mumeo, vumilia tu, ndoa ndivyo ilivyo." Wengine watamwambia "Umejua kututia aibu, watu wote wanatuangalia sisi, wanatusema, binti si kaolewa juzi juzi tu, leo amerudi!"

Kwa sasa hapo tena hiyo. Wanawake wa sasa wanajitambua na kwa bahati nzuri wamekuwa na uwezo mkubwa wa kujitafutia riziki wao wenyewe, hivyo wanaweza kujitunza bila msaada wa mwanaume.

"Ukimzingua anakuzingua." Wameelimika, wameendelea, wanajua haki zao na vitu vingi na wengi wamekuwa wajasiliamali tofauti na miaka ya nyuma mama na bibi zetu waliokuwa wakimtegemea mume tu.

Mwanamke ukimuoa leo kesho ukamzingua haoni tabu wala aibu kubeba kilicho chake akaondoka. Wala haimpi shida.

Hiyo inakupa picha wanaume hasa wa kizazi cha sasa kuishi nao kwa upendo na akili, na siyo kumfanya kama chombo tu cha kustarehe na kutompa matunzo au haki zake za msingi.

Leo tunautazama wimbo wa Orchestra Safari Sound (OSS), wakati huo wakitumia mtindo wa Dukuduku, chini ya uongozi wake, Freddie Ndala Kasheba. Wimbo unaitwa 'Ndoa za Siku Hizi

*"Mke wangu mama watoto hanitaki tena wowo, ndoa siku hizi ipo mashakani, yaani la kufanya sina oo, yeyeye, yeyeye, mke kudai talaka kama utani, yeyeye, yeyeye, mke kudai talaka kama utani.*

*Ndoa zamani zilikuwa na thamani, ilikuwa tamu wowowo, leo kwa wetu msimu ipo mashakani, haina umuhimu wo, yeyeye, yeyeye, mke kudai talaka kama utani, yeyeye, yeyeye, mke kudai talaka kama utani."*

Hapa mume anashangaa mkewe kudai talaka kama utani. Jamaa anasema ndoa siku hizi zipo mashakani siyo kama za zamani za 'kama hunitaki nirudishe kwetu'.

Na hii ni miaka ya katikati ya 1980 ujue, wanamuziki tayari walishaanza kuona mabadiliko kwenye ndoa. Sasa ndiyo kabisa. Zamani ilikuwa ngumu kuachana, leo hakuna, tena kama ukimchelewesha anaweza kuondoka, akakwambia 'utaniletea talaka yangu kwetu.'

"Mahari nimetoa kwa wazazi wake mama ooho, naona aibu mama kudai siwezi tena ooo, kwa vile sina baba sina mama wamekuwa kama wa kwangu ooo.

Mahari nimetoa kwa wazazi wake mama ooho, naona aibu mama kudai siwezi tena ooo, kwa vile sina baba sina mama wamekuwa kama wa kwangu ooo."

Jamaa pamoja kuachwa, lakini hawezi kwenda kudai mahari kwa sababu anawaheshimu sana wazazi wa mwanamke na amewafanya kama wa kwake. Ataanzia wapi? Hayo ndiyo mapenzi. Yana tamu na chungu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

# Kafie kwenu-1

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

KWA hali ya kawaida kijumba kile kilitakiwa kuwa banda la uani na si nyumba iliyojengwa peke yake.

Kikionekana kama kijumba kilichosahauliwa wakati zingine zikibomolewa. Watoto wa mjini wanasema imejegwa peke yake kama goli la mpira wa miguu.

Ni kweli Kinondoni Moscow kuna nyumba nyingi za kawaida sana na za hali ya chini, lakini hiyo ilikuwa inaongoza kwa uduni.

Ilijengwa kama behewa, na ilikuwa na milango mitatu ya nje. Ina maana mtu anayepanga hapo kama ana familia ni lazima apange vyumba viwili au vitatu. Kwa sababu kila chumba kimoja kilijitegemea.

Haikupigwa 'lipu', matofali yake yakiwa ni makuukuu, huku juu kukiwa na mabati yaliyobadilika rangi kutoka ya asili na kuwa meusi kwa sababu ya kukaa kwa muda mrefu na kuwa na kutu.

Juu ya mabati hayo kulikuwa na matairi makuukuu ya gari, pamoja na baadhi ya matofali ambayo yote kazi yake ilikuwa moja tu, kukandamiza au kuzuia mabati hayo yasing'oke kwa upepo, kwani misumari iliyopigiliwa mabati hayo, ilikuwa imechoka, na baadhi ilikuwa imeshang'oka.

Nje ya kijumba hicho kulikuwa na majani yaliyoota bila mpangilio na ilionekana anayeishi hapo, au wanaoishi ni wavivu kupindukia kufanya usafi na kurekebisha mazingira, au wasiokuwa na muda wa kufanya hivyo.

Angalau watu ambao wamelizoea banda hilo, hupita kama kawaida tu, lakini kwa wale ambao ni mara ya kwanza, ilikuwa ni lazima waliangalie mara mbili mbili.


Wengine hawakudhani kama mle anaweza kuishi binadamu badala yake waliona kuwa kama ni kijumba ambacho watu walishi zamani na wamehama.

Wapo waliodhani kama ni kuishi mtu basi atakuwa anaishi binadamu mwenye matatizo ya afya ya akili, na si mwenye akili timamu.

Wenye umri mdogo kidogo, watoto kuanzia miaka 15 kurudi chini huwa wakikiona kijumba kile, huangua vicheko.

Ghafla mlango ulifunguka. Aliyetoka ni kijana asiyezidi miaka 25. Hata hivyo alionekana kama ana zaidi kidogo ya umri huo kutokana na hali ngumu ya maisha aliyokuwa nayo.

Alikuwa amevaa pensi yake iliyochoka na fulana kuukuu. Mkononi alishika kikombe na bakuli. Alionekana kama mtu aliyetoka kunywa chai mida hiyo ya asubuhi.




**Walikuwa wanatembea kwa madaha mithili ya twiga mbugani. Kwa muda aliyowatazama alijikuta akipata burudani ya akili ya mwili. Ni kama presha yake ilikuwa imeshuka hivi. Mwili wake ulisisimka kama mtu ambaye anayesikiliza muziki mzuri anaoupenda.**

Alichofanya ni kuosha kikombe chake kwa maji ambayo yaliyokuwa kwenye bakuli. Kuosha kwenyewe ilikuwa ni kumwagua maji kikombe tu, bila sabuni wala kusuuza. Aliporidhika kwenye kuona ameosha, akarejea ndani.

Kwa bahati nzuri au mbaya, kwenye kijumba hicho aliishi yeye tu. Anaitwa James. Alikuwa anaishi kwenye chumba kimoja tu. Siyo kwamba alikuwa hana familia tu, lakini hata pesa yenyewe hakuwa nayo. Vyumba viwili havikuwa na mpangaji yoyote.

Alikuwa na miezi minne tu tangu ahamie kwenye kibanda hicho. Pamoja na hayo alizoeleka mapema mno kuliko hata baadhi ya watu waliohamia maeneo hayo miaka hata minne iliyopita.

Alikuwa mcheshi, lakini mpole. Alionekana kuwa na nidhamu kubwa, adabu kwa watu wa rika zote kiasi cha kupendwa hata na wazee.

Wao walishangaa kuona kijana wa aina ile ana adabu kama waliokuwa nao wao zamani. Kwa miaka ya hivi karibuni hawajawahi kuona kijana kama huyo.

Pamoja na yote hayo, hawakuzuia au kupooza ile hali ya ufukara aliyonayo, licha ya mara kwa mara kumpa chakula, pesa ndogo ndogo na zawadi zingine ambazo zilimfanya tu kupitisha njaa na shida ya siku moja, mbili au tatu na si kujikwamua kabisa.

James hakuchagua kazi. Na hiyo ndiyo sababu iliyomfanya kujulikana kirahisi na kwa haraka zaidi. Kuokota makopo na kwenda kuuza, kuzoa taka, kutapisha vyoo, na kazi zingine ndogo ndogo za majumbani ambazo ujira wake ni wa kwaida tu usiomuwezesha kupiga hatua yoyote mbele. Moyoni mwake hakuzipenda kazi hizo, lakini alizifanya kwa bidii kubwa.

*************************************

Akiwa anatoka kununua mihogo ya kukaanga kwa mama binti Mshindo, alikatisha kichochoro kimoja na kukutana na wasichana wawili. Alisimama na kuwatazama. Ni kama walifanana hivi. Lakini macho yake yakaganda zaidi kwa mmoja bila sababu yoyote ile.

Walikuwa wanatembea kwa madaha mithili ya twiga mbugani. Kwa muda aliyowatazama alijikuta akipata burudani ya akili ya mwili. Ni kama presha yake ilikuwa imeshuka hivi. Mwili wake ulisisimka kama mtu ambaye anayesikiliza muziki mzuri anaoupenda.

"Hawa ni binadamu, au malaika," alijiambia mwenyewe. Mpaka wakati huo alikuwa amesimama. Hakuna na nguvu za kutembea. Alikuwa amesimama pembeni kama mtu ambaye alikuwa anawapisha wapite.

Ndiyo muda ambao alipata wasaa wa kuwatazama vizuri warembo hao. Kila walipokuwa wakikaribia harufu ya manukato ilizidi kumchanganya.

Akiwa na bakuli lake lililojaa mihogo alibaki ameduwaa mpaka wasichana hao walipomfikia.

"Habari zenu warembo."

Hakusikia sauti yoyote iliyomjibu. Mmoja alimtazama kuanzia chini, akampandisha hadi juu. Macho pekee yalikuwa na sauti tosha. Waliongea. Hakupenda kabisa salamu hiyo. Alipomaliza kumtazama kwa dharau, akaishia na kufyonya.

Mmoja aliyebaki hakujibu chochote na wala hakuitikia salamu. Alibaki anamtazama mwenzake.

James hakujali, kukasirika wala kupata presha kwa kilichotokea. Wala hakujibu fyonyo hilo kwa maneno makali au hasira.

Alibaki kimya na kutabasamu. Kwa maisha anayoishi James, hilo kwake ni jambo alilolizoea kabisa. Ameshawahi kudhalilishwa mara 10 zaidi ya alivyofanya yule msichana. Ameshawahi kumwagiwa mpaka maji ya ukoko na mambo mengine mengi ambayo yamebaki kuwa siri yake moyoni.

Kwa ufukara na muonekano wake hilo ni jambo la kawaida sana. Ni kama msichana yule hakufanya kitu chochote ambacho kingemkasirisha James. Kama msichana yule alifanya vile ili kumkasirisha alikuwa amenoa.

ITAENDELEA JUMAPILI

# BEYONCE, KELLY KUWAJENGEA NYUMBA MASKINI

WANAMUZIKI wawili waliokuwa wakiunda kundi la Destiny's Child, wameishangaza dunia baada ya kutangaza kujenga nyumba 31 kwa ajili ya kuwasaidia watu wasiokuwa na makazi.

Wasanii hao,Beyonce na Kelly Rawland, watajenga nyumba hizo katika kaunti ya Harris katika eneo la Midtown la Houston.

Aidha, sehemu ya pesa hizo kiasi cha dola milioni saba zitapelekwa katika makazi ya Knowles-Rowland kama mpango wa uokoaji wa Marekani.

"Kaunti ya Harris na jiji la Houston, kwa pamoja na muungano wa watu wasio na makazi, wamepunguza ukosefu wa makazi katikati ya janga hilo kwa asilimia 20, na tumeweza kushikilia upungufu huo," Jaji Lina Hidalgo amesema katika mkutano na waandishi wa habari.

Ameongeza "Ni mipango kama hii ambayo hakika nitaiunga mkono bila kujali ni nani aliye nyuma yake, lakini inavutia sana, nadhani, kwa sababu kuna majina haya ya Beyoncé na Kelly Rowland, bila shaka, wamekuwa wakiunga mkono. jamii kwa muda mrefu sana."

Hidalgo mesema kuwa uzinduzi utatangazwa wakati wa tamasha la Renaissance World Tour itakapofanyika Oktoba huko Houston.






## Amosi Acrobatics anafurahia burudani ya kujinyonga mwili

MSANII wa burudani inayoambatana na sarakasi, Amos Acrobatics, amesema sanaa hiyo inazidi kukua kwa kasi na inaweza kupata umaarufu ndani ya miaka michache.

Akizungumza na Nipashe, Amos amesema kwa upande wake anajivunia kufanya kazi hiyo na ana uhakika ndani ya miaka michache atapata mafanikio makubwa.

"Sanaa hii ni ngumu na ndio maana watu wengi wanakwepa kufanya, lakini nina uhakika ndani ya miaka michache nitapata mafanikio makubwa hasa kutokana na watu wengi wanapenda kuangalia," amesema Amos.

## ZISIKUPITE

### BARNES ATAKIWA NEWCATLE

KLABU ya Newcastle United inatumai kuwa inaweza kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 35 kwa winga wa Leicester City, Harvey Barnes ili kuzipiku Aston Villa na West Ham kuipatasaini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 25. (***Guardian***)

### MABPPE NA PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe anafikiria kuwa huenda akalazimika kuondoka Paris St-Germain msimu huu wa joto kwani bado hana mpango wa kuongeza mkataba wake zaidi ya mwaka 2024 na chaguo la timu ambayo anapenda kujiunga nayo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ni Real Madrid. (***ESPN***)

### PSG YAMSHTUKIA MBAPPE

KLABU ya PSG inaamini Kylian Mbappe tayari amekubali kujiunga na Real Madrid kwa uhamisho wa bila malipo msimu ujao wa joto na, ikiwa hatasaini mkataba mpya na mabingwa hao wa Ufaransa, watamuuza kwa dau la juu zaidi msimu huu wa joto. (***Sky Sports)***

### ARSENAL CHAGUO LA KWANZA

CHAGUO la kwanza la Kylian Mbappe ikiwa angehamia Ligi Kuu ya England litakuwa Arsenal, lakini yuko nje ya bajeti ya Washikabunduki na hakuna mawasiliano yaliyofanywa kati ya pande hizo mbili. (I***ndependent***)

### FELIX AITAKA PSG

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Joao Felix anataka kuhamia PSG, lakini anaweza kuishia kubakia Atletico Madrid, ambao wanataka euro milioni 100 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 23. (***AS***)

### LLORIS ATAKIWA MAN

KLABU ya Inter Milan inaongeza bidii katika kumsaka mlinda mlango wa Tottenham Hotspur, Hugo Lloris mwenye umri wa miaka 36, huku wakipanga Mfaransa huyo achukue nafasi ya mchezaji wa kimataifa wa Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 27, ambaye analengwa na Manchester United. ***(Foot Mercato)***

### GYOKERES SAFI

KLABU ya Sporting Lisbon imekubali mkataba wenye thamani ya euro milioni 24 na Coventry City kwa mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 25. (***Fabrizio Romano)***

### SIMEONE AKATAA

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone amekataa ofa nono ya kuwa kocha wa klabu ya Al Ahli ya Saudi Arabia ili kubakia na timu hiyo ya Hispania. ***(ESPN***)

### DELE AMEREJEA

KIUNGO wa kati wa England, Dele Alli amerejea mazoezini na Everton huku akilenga kurudisha kiwango chake kwenye mstari, ambapo kocha wa Toffees hao, Sean Dyche amemwambia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuwa anahitaji "kujiweka sawa". (***Mail***)

### TOURE ATAKIWA

KLABU ya Everton imeiambia Almeria kwamba wanayo nia ya kufikia kipengele cha kuachiwa kwa El Bilal Toure cha euro milioni 40, ingawa Fulham wanaweza kumnunua mshambulizi huyo wa Mali mwenye umri wa miaka 21, ikiwa watamuuza mshambuliaji wa Serbia, Aleksandar Mitrovic mwenye umri wa miaka 28 msimu huu wa joto. (***Sacha Tavolieri)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: SITAONGEZA MKATABA MPYA PSG

**Anafikiria kuondoka katika kipindi hiki cha usajili huku Real Madrid likiwa chaguo lake la kwanza...**

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe bado hana mpango wa kuongeza mkataba wake zaidi ya Juni 2024 katika klabu ya Paris Saint-Germain licha ya tishio kutoka kwa Rais wa klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi, na anaanza kufikiria kuwa atalazimika kuondoka msimu huu, huku Real Madrid likiwa chaguo lake, kwa mujibu wa ESPN.

**Matamshi ya Al-Khelaifi hayajamfurahisha au kumtisha fowadi huyo wa PSG, vyanzo viliiam bia ESPN na kwamba Mbappé, ambaye yuko Cameroon kwa siku tatu za likizo, amepuuuzia kuhusu hali hiyo.**

Real Madrid inabakia na matumaini ya kuweza kukamilisha dili ambalo wanakadiria litakuwa na thamani ya zaidi ya euro milioni 200, lakini wanataka Mbappé au PSG kuchukua hatua ya kwanza kabla ya mazungumzo kuanza rasmi.

Madrid wanataka kuepuka tukio la majira ya joto lililopita pale nahodha huyo wa Ufaransa alipoamua kusaini mkataba mpya na PSG dakika za mwisho licha ya Madrid kuwa na uhakika kwamba ujio wake ulionekana kukamilika.

Mkakati wa timu na rais wa Madrid, Florentino Pérez ni kuweka hadhi ya chini na kusubiri Mbappé au PSG kuchukua hatua ya kwanza kuelekea uhamisho kabla ya kuweka dau la uhakika la kusaini.

Madrid ndio klabu pekee ambayo Mbappé anataka kujiunga nayo msimu huu wa joto, vyanzo viliiambia ESPN, na ndio timu pekee inayoweza kumnunua.

ESPN iliripoti kwamba wababe hao wa LaLiga wana kila kitu kikiwa tayari watakapopata taa ya kijani kutoka kwa Mbappé au PSG. Wanafahamu kuwa mpango huo utazidi euro milion 200 kutokana na ada, nyongeza na kamisheni.

Kulingana na vyanzo vya ESPN, hakujakuwa na mawasiliano kati ya klabu hizo mbili, lakini Madrid wamekuwa wakizungumza na wawakilishi wa Mbappé.

Mwezi uliopita, Mbappé alisema hadharani kwamba anataka kubakia PSG kwa msimu mwingine lakini Al-Khelaifi alikuwa wazi wiki hii na kutoa kauli ya mwisho kwa mchezaji wake nyota.

"Kylian lazima aamue baada ya wiki moja au mbili zaidi. Ikiwa hatasaini mkataba mpya, tutamuuza. Sio mazungumzo," Al-Khelaifi alisema Jumatano katika mkutano wakati wa utambulisho wa kocha Luis Enrique.

Mbappé hajawahi kuahidi PSG kwamba hataondoka kama mchezaji huru, lakini angependelea kuondoka huku klabu ikipokea ada ya uhamisho ili wapate fedha za kusajili mbadala wake.

## Man Utd kuamua mustakabali wa Greenwood

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inalenga kufanya uamuzi juu ya mustakabali wa Mason Greenwood kabla ya kuanza kwa msimu mpya, vyanzo vimeiambia ESPN.

Greenwood hajaichezea klabu hiyo tangu Januari 2022 kufuatia kukamatwa kwake kwa tuhuma za kujaribu kubaka na kushambulia.

Mashtaka ya uhalifu yalitupiliwa mbali Februari, lakini alibakia kusimamishwa huku United ikianzisha uchunguzi wao wa ndani.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba mchakato huo unakaribia kukamilika na Greenwood atajua hatima yake kabla ya United kuanza msimu mpya dhidi ya Wolves pale o Old Trafford Agosti 14.

Greenwood hakuwepo kwa timu hiyo kuanza mazoezi ya kujiandaa na msimu Alhamisi lakini amekuwa akifanya mazoezi peke yake katika juhudi za kuimarisha utimamu wake.

Mchezo wake wa mwisho kwa United ulikuwa wa ushindi wa 1-0 dhidi ya West Ham United Januari 22, 2022.

Bila kujali kama Greenwood anaruhusiwa kujiunga na kikosi tena, Erik ten Hag atalenga mshambuliaji mpya msimu huu wa joto.

Harry Kane na Victor Osimhen wameonekana kutoweza kufikiwa kwa sababu ya tathmini zilizowekwa na Tottenham na Napoli, huku Rasmus Hojlund wa Atalanta na Randal Kolo Muani wa Eintracht Frankfurt wakiibuka kama walengwa wanaopendelea.

United wanafanya kazi na bajeti ndogo msimu huu wa joto na baada ya kutumia pauni milioni 55 kununua Mason Mount.




# POCHETTINO ATAKA KUSHINDA KILA MECHI




**LONDON,** England

KOCHA mpya wa Chelsea, Mauricio Pochettino amesema anajua tayari yuko kwenye shinikizo katika jukumu lake jipya, akiri matarajio ya mara moja pale Stamford Bridge ni kushinda licha ya ugumu wa klabu msimu uliopita.

Kumaliza kwa Chelsea katika nafasi ya 12 wakiwa na pointi 44 kwenye kampeni za mwisho ilikuwa ni kiwango kibaya zaidi tangu mwaka 1994 kwani walikuwa na wakati mgumu chini ya makocha watatu -- Thomas Tuchel, Graham Potter na bosi wa muda Frank Lampard.

Lakini Pochettino alielezea kile kinachotarajiwa kutoka kwake katika mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari tangu aanze kuinoa Stamford Bridge Julai Mosi.

"Lengo langu ni kushinda, nia yangu ni kushinda. Kucheza vizuri ni mtindo wetu, falsafa na utamaduni wetu. Ikiwa hutashinda katika klabu kama Chelsea inakuwa ni jambo gumu," alisema Pochettino.

"Kwa wachezaji tulionao na mkakati wa kuamini. Ni juu ya kushinda, kuwa na ushindani. Na kutafsiri nguvu hii kwa mashabiki wetu. Ili kuunda umoja, ni ngumu, katika Ligi Kuu kwa pamoja tunaweza kukaribia kushinda tena. "

Pochettino hapo awali alifurahia kuwa kwenye Ligi Kuu akiwa na Southampton na Tottenham Hotspur ambayo aliiongoza hadi fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019 kabla ya kuondoka bila taji miezi mitano tu baadaye.

Kocha huyo wa Argentina alisema hatarajii subira zaidi kwa Chelsea -- klabu ambayo imekuwa imepitiwa na makocha wengi katika miongo miwili iliyopita.

"Katika soka, ni vigumu kusubiri," aliongeza. "Chelsea inahitaji kufanya kazi kuanzia siku ya kwanza. Tunachofanya sasa kwenye uwanja wa mazoezi ni juu ya kufanya kazi kuanzia sasa, ili kujituma zaidi. Soka ni leo au jana. Hatuwezi kuzungumza kwa muda mrefu. Hatuwezi kuwaambia watu tunachohitaji, miezi sita, nadhani sio nzuri. Tutakuwa na kikosi cha wachezaji ambao wanaweza kufanya kazi."

Kikosi cha Chelsea kinakabiliwa na msukosuko katika kipindi hiki cha majira ya joto, huku wachezaji tisa waandamizi wakiondoka klabuni hapo, akiwemo Kai Havertz kwenda Arsenal na Mason Mount kwenda Manchester United.

Klabu hiyo pia iko kwenye mazungumzo juu ya kuwaachia wachezaji zaidi, na vyanzo vimeiambia ESPN kwamba AC Milan iko kwenye mazungumzo ya kumsajili Christian Pulisic.

Hata hivyo, Pochettino alisema idadi kubwa ya wachezaji wanaoondoka haimhusu..

# Simeone aikataa ofa nono ya Saudia

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Atlético Madrid, Diego Simeone amepokea ofa nono kutoka klabu ya Al Ahli ya Saudi Aarabia, lakini vyanzo vimeiambia ESPN kuwa hana mpango wa kuachana na kazi yake kule kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Marca iliripoti Ijumaa kwamba Al Ahli, moja ya klabu za juu za Saudi Pro League, imewasiliana na kocha huyo wa Argentina na ofa "kubwa ", lakini vyanzo vya ESPN vimesema atabakia Madrid.

Vyanzo hivyo pia vilisema hii si mara ya kwanza kwa klabu hiyo ya Saudia kuuliza kuhusu huduma ya Simeone na kwamba ofa nono pia iliwasilishwa Mei.

Simeone alitia saini mkataba wa nyongeza miaka miwili iliyopita ambao utamfikisha mwisho wa msimu wa 2024 na amedokeza kuwa angependa kuendelea na klabu hiyo.

Licha ya matatizo mapema msimu huu, Simeone aliifufua timu hiyo na wakamaliza katika nafasi ya tatu katika ligi ya Hispania msimu huu uliopita, nyuma ya mabingwa Barcelona na Real Madrid, hivyo kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2023/24 kwa mara ya 11 mfululizo.

Atletico wameunda upya kikosi msimu huu wa joto, na kuwaongeza Javi Galán, Çağlar Söyüncü na César Azpilicueta.

Simeone amekuwa kocha wa Atletico tangu mwaka 2011, na kumfanya kuwa mtu ambaye amefundisha timu kwa misimu mingi mfululizo kwenye LaLiga.

Simeone mwenye umri wa miaka 53 alifundisha River Plate miongoni mwa klabu nyingine za asili yake Argentina na alikuwa na muda mfupi katika klabu ya Italia Catania kabla ya kuchukua mikoba ya Atlético.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Álvaro Morata pia amepokea ofa kutoka kwa klabu ya Saudi pamoja na nia kutoka kwa AC Milan.



# SULEIMAN JABIR RAIS MPYA ZFF

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wamemchagua Suleiman Mohmed Jabir kuwa Rais mpya wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF ) kwa kipindi cha miaka minne.

Jabir amechaguliwa kwa kupata kura 16 sawa na asilimia 51 katika Uchaguzi uliofanyika jana hapa Visiwani Zanzibar.

Katika uchaguzi huo ambao ulikuwa na wagombea watatu, Kamal Abdulsatar alipata kura15 sawa na asilimia 49 wakati Juma Thabit hakupata kura.

Akizungumza mara baada ya kutangazwa kuwa mshindi, Jabir alisema lengo lake kuu akianza majukumu yake ni ni kuhakikisha Mpira wa Zanzibar unasonga mbele.



Alisema atahakikisha anafanya kazi kwa ukaribu mkubwa na Wajumbe pamoja na wadau wa soka ili kuhakikisha Zanzibar inarudisha hadhi yake katika Soka kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

"Nawashukuru Wajumbe wote walionipigia kura na wale ambao pengine hawakunipigia kura hiyo ni demokrasia hivyo sote tutashirikiana kwa pamoja kuona soka la Zanzibar lisonga mbele, nitaendelea pale walipoishia wenzangu pamoja na kusonga mbele ili kuyafikia malengo yetu"alisema Jabir.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi huo, Fadhil Ramadhan Mberwa akizungumza mara baada y'a kumtangaza mshindi huyo alimtaka Rais huyo mpya wa ZFF kufanya kazi zake kwa kufuata katiba ya shirikisho hilo ili kuepuka mivurugano na migongano inayozorotesha mpira wa miguu Zanzibar.

Alisema, ili kukwepa mivurugano ni lazima kufanya kazi kwa kuhakikisha katiba ya ZFF inasimamiwa ipasavyo na kufuata kanuni zote ambazo.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Lake Energies, Abdirahman Ahmed akipiga mpira wa gofu, kwenye mashindano ya mchezo huo yaliyofanyika juzi kwenye viwanja vya Gymkhana, Dar es salaam. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# *Mashindano Gofu Lake Energies yafana Dar*

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa wanawake wacheza gofu nchini (TLGU), Queen Siraki, amesema mashindano ya gofu yaliyofanyika juzi kwenye viwanja vya Gymkhana ya 'Lake Energies' yameongeza hamasa kwa wachezaji wa mchezo huo.

Akizungumza muda mfupi baada ya kumalizika mashindano hayo yaliyoshirikisha wachezaji wa ridhaa, wachezaji wa kulipwa na watoto, Queen alisema ujio wa lake Energies kudhamini mchezo huo umeongeza ushindani kwa wachezaji.

"Mashindano haya yameleta ushindani mkubwa sana na tunatamani lake Energies waendelee kutudhamini kwenye mashindano mengine, tumeshuhudia walimu wetu wanaotufundisha hapa Gymkhana wakishindana wenyewe kwa wenyewe na kutoa somo kwa vijana wengi, kiufupi mashindano haya yamefana sana," alisema Queen.

Kwa upande wake , Mkurugenzi Mtendaji wa Lake Energies, Abdirahman Ahmed, alisema kampuni huiyo itaendelea kusapoti mchezo huo na wanafikiria kudhamini mashindano ya 'Co-operate' yanayotarajiwa kufanyia mwezi ujao.

"Nawashukuru wote walioshiriki mashindano haya, sisi kama Lake Energies tutaendelea kusapoti michezo kwa sababu tunaamini michezo inaleta umoja na pia ni namna moja wapo ya kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuinua michezo nchini," alisema Ahmed.

Katika mashindano hayo kwa upande wa wachezaji wa kulipwa, Frank Mwinuka aliibuka mshindi wa jumla kwa kupata grosi 71na kukabidhiwa zawadi ya pesa shilingi milioni moja akifuatiwa na Salum Dilunga (grosi 73) ambaye alipata Sh, 664,000 wakati nafasi ya tatu ikishikwa na Rodrick John (grosi 74) na kuzawadiwa Sh. 420,000.

Mbali na fedha hizo, pia washindi walikabidhiwa mitungi ya gesi kutoka kwa kampuni hiyo.

# Gamondi afunguka

INATOKA UK. 24

Katika hatua nyingine Uongozi wa klabu hiyo umemsainisha mkataba wa miaka mitatu beki wa timu ya Taifa ya Uganda, Gift Fred ili kuitumikia kuanzia msimu ujao.

Fred amesajiliwa na Yanga baada ya kumaliza mkataba wake kwenye klabu ya nyumbani kwao ya SC Villa.

Wakala wa mchezaji huyo Ivica Stankovic aliiambia Nipashe kuwa mazungumzo na Yanga yameenda vizuri na wamekubaliana kusaini mkataba huo wa miaka mitatu.

"Kila kitu kimeenda sawa, naweza kusema Fred ataichezea Yanga msimu ujao," alisema Stankovic.

Yanga ilianza kumfuatilia mchezaji huyo wakati wa mchezo wa timu yake ya taifa dhidi ya Algeria wa kuwania kufuzu fainali za Afcon, mchezo huo ulichezwa Cameroon.

# Robertinho aridhishwa usajili Simba

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Robert Oliveira 'Robertinho' amesema amefurahishwa na usajili unaoendelea kufanywa na viongozi wa timu hiyo kwa kuwa umefuata mapendekezo yake.

Robertinho alisema katika maandalizi yake kuelekea kwenye msimu mpya, anataka mechi tatu za majaribio wakiwa nchini Uturuki watakapokwenda kuweka kambi.

"Tumefanya usajili wa nguvu ili kuleta uwiano sawa kwenye maeneo tofauti, tunajua ubora tuliokuwa nao msimu uliopita lakini tunataka kuwa bora zaidi kulingana na malengo tuliyonayo ili kuvuka vikwazo vilivyotukwamisha msimu uliopita, nina furaha usajili wa wachezaji ambao wametambulishwa na nilikuwa nikifahamishwa kila kitu kilichokuwa kikiendelea, viongozi wamefanya kazi kubwa sana, sasa ni wakati wetu wa kujiandaa na kutafuta uwiano wa wachezaji kama timu," alisema kocha huyo wa zamani wa Vipers ya Uganda.

Mpaka sasa Simba imetambulisha wachezaji wawili ambao ni Willy Essomba Onana raia wa Cameroon akitokea Rayon Sport ya Rwanda, Aubin Kramo Kouame kutoka Asec ya Ivory Coast na Fabrice Ngoma.

Kwa mujibu wa Robertinho golikipa Caíque Luiz Santos anayekipiga kwenye klabu ya Ypiranga SC anatarajiwa kutua nchini leo kwa ajili ya kusaini mktaba wa kuichezea Simba.

"Atakuja kipa kesho (leo)," alisema kocha huyo, huku akiweka wazi mipango yake ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.

"Maandalizi yetu yatakwenda sambamba na michezo ya kirafiki tukiwa Uturuki, tukiwa huko natarajia kupata mechi tatu za kirafiki kwa ajili ya kutengeneza timu ili iwe na muunganiko mzuri," alisema.

Wakati huo huo, mcheza jimpya wa Simba, Kramo alieleza kufurahishwa kwake kujiunga na timu hiyo na kuwaomba mashabiki wa timu hiyo kujaa viwanjani kama kawaida yao wakati timu yao inacheza.

"Mashabiki wa Simba, nimefurahi sana kujiunga na timu hii, tutaanza kuonana viwanjani hivi karibuni, natarajia watakuja kwa wingi na watajaa kama ilivyo kawaida ili kutushuhudia," alisema mchezaji huyo anayecheza winga zote mbili pamoja na nafasi ya mshambuliaji.

Michezo
Jumapili Julai 9, 2023
Nipashe



## Mbappe: Sitaongeza mkataba PSG




Mashabiki wa klabu ya Yanga wakiwa wameshika jezi mpya za timu hiyo ndani ya viwanja vya maonyesho ya biashara (Sabasaba) jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Ni vita Ngao ya Jamii

## ●●● Simba, Yanga kusaka fainali, mechi kuchezwa Agosti 9 Mkwakwani...

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), limetoa ratiba ya mechi za Ngao ya Jamii, kuashiria kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu ambapo Yanga na Simba zitasaka nafasi ya kucheza fainali kwa kuumana na Azam na Singida Fountain Gate Agosti 9 na 10.

kufanyika kwa michezo hiyo ya kusaka mshindi wa ngao ya jamii ni kiashiria cha kufunguliwa pazia la Ligi Kuu kwa msimu wa 2023/2024 ambapo utaanza wiki moja baada ya michuano hiyo ya kuwania bingwa wa Ngao ya Jamii.

Msimu huu TFF imebadilisha utaratibu uliozoeleka wa bingwa wa ligi kuu kucheza na bingwa wa kombe la Shirikisho FA kusaka mshindi wa Ngao ya Jamii.

**Msimu huu timu nne za Yanga, Simba, Singida na Azam zitaumana kusaka timu mbili zitakazo shiriki fainali ya kusana bingwa wa ngao ya jamii kwa mismuwa 2023/2024.**

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana na na TFF, Yanga itacheza na Azam FC Agosti 9 kwenye Uwanja wa Mkwakwani kabla ya Simba kuumana na Singida Fountain Gate Agosti 10 kwenye uwanja huo.

Washindi kwenye kila mchezo watacheza fainali Agosti 13 kwenye uwanja huo kumpata bingwa wa ngao ya jamii.

Aidha, kabla ya mchezo huo wa fainali kutakuwa na mechi ya kusaka mshindi wa tatu kwa timu zilizofungwa au kutolewa kwenye mechi za awali.

TFF, ilitangaza mabadiliko ya mfumo wa kumsaka mshindi wa Ngao ya Jamii kwa kile ilichoeleza kuondoa timu kujirudiarudia kila msimu na pia kufanya kuwa na msisimko zaidi.

Hii itakuwa kwa mara ya kwanza Ngao ya Jamii kuchezwa kwa mfumo huo mpya ambapo zitakuwa zikichukuliwa timu nne za juu, kuanzia bingwa hadi aliyeshika nafasi ya nne na kucheza kwa mtindo wa mtoano.

Kwa kawaida baada ya michezo ya Ngao ya jamii wiki moja baadae pazia la ligi kuu linafunguliwa rasmi, kwa mantiki hiyo ligi kuu Tanzania bara msimu wa 2023/2024 inatarajiwa kuanza Agosti 20.

# Gamondi afunguka kujiunga Yanga SC

**Na Saada Akida**

KOCHA Miguel Gamondi amesema licha ya kuwa na ofa ya kujiunga na klabu kadhaa za Misri na Saudi Arabia, mafanikio na mipango endelevu ya Yanga ndio sababu ya kuamua kujiunga nayo.

Akizungumza na Nipashe muda mfupi baada ya kuwasili nchini tayari kwa majukumu yake mapya, Gamondi alisema kabla ya kusaini mkataba wa kukubalia kikosi cha timu hiyo alikutana na Rais wa Yanga, Hersi Said na kuainisha mipango yao ambayo ilimvutia na kukubali kuchukuwa jukumu la kukinoa kikosi cha mabingwa wao wa Tanzania.

"Mbali na mpango yao lakini Yanga ni timu kubwa na imefanikiwa kucheza fainali ya kombe la Shirikisho Afrika (CAF), imechangia mimi kukubali kupokea hii kazi ili kuhakikisha tunaendeleza pale ilipoishia ikiwemo kutwaa mataji na kufanya vizuri kimataifa," alisema Gamondi.

Alisema atahakikisha anaitoa yanga ilipoishia msimu uliopita na kuipeleka mbele zaidi.




INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042